SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Prof.** Ngowi azikwa, wataka machapisho yake kutumika

UKURASA 3




JOAO ANAFANYA KILA KITU ATLETI - SIMEONE

UKURASA 22


# Nipashe

Jumatatu Aprili 4, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580905

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The G... nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US




# Wachungaji KKKT waanza kufurumushwa

UKURASA 16



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (watatu kulia), akiongoza ujumbe wa mawaziri wa wizara za kisekta baada ya kutua na helikopta mkoani Tanga walipokwenda kutoa mrejesho wa utatuzi wa migogoro ya ardhi katika vijiji 975. **Habari Ukurasa 4. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wajasiriamali walia kupaa kwa ngano, mafuta

UKURASA 2

## Mama ajitosa mtoni kumwokoa mwanawe asiliwe na mamba

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 7

**ZITTO AKABIDHI KITI KWA KINANA**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amemaliza muda wake wa uongozi kwa nafasi ya...

MICHEZO STARS IMENIONGEZEA VITU - MPOLE UK.23 MAONI, KATUNI UK.6



Rais wa Baraza la Biashara barani Afrika, Dk. Amany Asfour (kushoto), akimkabidhi zawadi Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, wakati wajumbe wa viongozi wa Chemba za Biashara tofauti sita (Misri, Zambia, Botswana, Rwanda, Burundi, Ethiopia na Uganda) walipotembelea makao makuu ya Benki ya CRDB. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajasiriamali walia kupaa ngano, mafuta

**Na Jenifer Gilla**

BEI ya unga wa ngano na mafuta ya kula imeendelea kupaa, huku wajasiriamali na wakazi kadhaa wa Mkoa wa Dar es Salaam wakielezea hali ngumu ya maisha kutokana na kuongezeka kwa gharama hizo.

Athnat John (45) mfanyabiashara wa maandazi Tabata alisema kuwa alilazimika kusimamisha biashara hiyo kwa kuwa anafanya biashara kwa hasara kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta na unga wa ngano.

"Nimeamua kusimama kwanza mpaka mafuta na unga wa ngano vitakaposhuka bei maana napata hasara, nilijaribu kupandisha maandazi kutoka Sh.100 hadi 200 lakini mwitikio ulikuwa mdogo sana, nikawa nauza maandazi 10 kati ya 200," anasema Athnat.

Kwa mujibu wa Athnat, lita moja ya mafuta aina ya Korie kwa sasa inauzwa Sh. 7,000 kutoka Sh. 5,500 waliyokuwa wakinunua wiki tatu zilizopita huku unga wa ngano sasa wananunua Sh. 2,000 kwa kilo moja kutoka Sh. 1,700.

Naye Amina Salum mkazi wa Boko anayefanya biashara ya kuuza chapati, alisema kuwa biashara inayumba kutokana na kupandisha bei ya bidhaa hiyo kutoka Sh. 250 hadi 400 kwa sasa hali inayosababisha wateja kuhama.

"Tangu nimepandisha bei ya chapati wiki mbili zilizopita wateja wamekata mguu, kwa siku nikiuza sana ni chapati 20 kati ya 150 nilizokuwa nauza hapo mwanzo, kwa hiyo hapa nawaza nifanye biashara gani itakayotoka maana nina watoto wanaonitegemea," alisema Amina.

Anasema sasa hivi wateja wengi wanaokwenda kwenye biashara yake huishia kunywa supu tupu au maharagwe makavu bila chapati na wengine kuja na vitafunio vyao kama vile mikate ambayo bado haijapanda bei.

Naye James Lamerk mfanyabiashara wa chips eneo la Temeke alisema kuwa amelazimika kupunguza kipimo, ili kufidia mafuta ambayo ananunua dumu la lita 20 kwa Sh. 125,000 kutoka 108,000.

"Nimeona nikipandisha bei nitafukuza wateja wangu kwa hivyo bei ni ileile ya Sh.1,500 sahani, lakini nimepunguza kidogo kwa hiyo mteja mwenyewe ataamua ale sahani ngapi kulingana na uwezo wake," alisema Lamerk.

Muuza duka la jumla eneo la Mwenge ambaye hakutaka kutaja jina lake, alisema kuwa wanalazimika kupandisha bei ya bidhaa kwa sababu hata wao wananunua ghali.

"Si umesikia rais mwenyewe katangaza kuwa vita ya Ukraine inaathiri upatikanaji wa mafuta kwa hiyo bidhaa zitapanda, kwa hiyo mimi sina jinsi, wakipandisha na mimi napandisha, nikiona mambo magumu basi nitarudi kijijini kulima, sasa nitafanyaje," analalamika.

Wiki iliyopita, wakati akipokea ripoti ya CAG Ikulu Dodoma, Rais Samia Suluhu alisema kuwa kwa sasa bidhaa zitapanda bei kutokana na vita ya Ukraine kusababisha kupanda kwa usafirishaji wa bidhaa na kuwaagiza watendaji wake waambie ukweli wananchi.

"Nauli zitapanda, usafirishaji wa bidhaa zitapanda. Sasa hivi kutoa kontena China ya bidhaa kuleta Tanzania walikuwa wanalipa kontena ya ft 40 dola 1,500, sasa hivi ni dola 8,000-9,000. Hii inaenda kuingia kwenye bidhaa anazozileta kwahiyo waambieni wananchi ukweli, wasikae tu kulaumu serikali haisemi kitu," alisema Rais Samia.

Kuhusu bei ya mafuta ya kula aliagiza tathmini ya tozo iliyowekwa kwenye bidhaa hiyo inayotoka nje, ili kulinda viwanda vya ndani iangaliwe upya kwa kuwa viwanda hivyo vya ndani havizalishi.

Akizungumzia mafanikio ya wizara yake kwa kipindi cha miaka 100 ya uongozi wa Rais Samia Machi 16, mwaka huu, Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, pamoja na mambo mengine alisema serikali imekuwa ikichukua hatua ya kukabiliana na kupanda kwa bei ya baadhi ya bidhaa ambazo zimekuwa zikipandisha gharama za maisha.

Alisema kupanda kwa bidhaa hizo hakutokani na sera za ndani, uzembe au uamuzi wa serikali bali ni majanga yanayoikumba dunia ikiwamo vita ya Urusi na Ukraine pamoja na ugonjwa wa UVIKO-19.

Alizitaja baadhi ya bidhaa ambazo zimepanda kutokana na majanga hayo kuwa ni zinazoagizwa kutoka nje kama vile ngano, mafuta ya kupitia, mbolea, mafuta ya mitambo na magari na vifaa vya ujenzi.

Alitolea mfano wa unga wa ngano ambao kabla ya UVIKO-19, Machi 2019 yalikuwa yanauzwa kwa Sh. 100,000 kwa kilo moja lakini sasa kutokana na ugonjwa huo pamoja na vita umefika Sh. 140,000 kwa kilo moja, huku mafuta ya mawese yakiuzwa Sh. 5,600 kwa lita kutoka Sh. 3,000.

Hata hivyo , Jan 24, mwaka huu, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Dk. Ashatu Kijaji, alisema serikali haitavumilia tabia ya wafanyabiashara wachache wenye dhamira ovu ya kuwaumiza wananchi kwa kujiamulia kupandisha bei za bidhaa bila kufuata utaratibu kwa manufaa yao binafsi.

Alisema kwa kuwa serikali inajukumu la msingi la kusimamia ushindani wa haki kwenye soko kwa kudhibiti mienendo hadaifu au kandamizi ya wazalishaji wa bidhaa na wafanyabiashara wanaopandisha holela wa bei za bidhaa nchini.

Waziri Kijaji aliyasema hayo alipokuwa akitoa taarifa ya uchunguzi uliofanywa na FCC, kuhusu uhaba na kupanda kwa bei za vinywaji baridi uliotokea Oktoba hadi Januari 2022 ulitokana na kutopatikana kwa sukari ya viwandani sababu ya ukosefu wa makasha ya kusafirishia shehena ya sukari hiyo kuja hapa nchini uliojitokeza duniani kote kutokana na athari za UVIKO-19.

# Mama ajitosa mtoni, amwokoa mwanawe asiliwe na mamba

**Na Said Hamdani**, LINDI

MKAZI wa Kijiji cha Sinde, Kata ya Mchinga mkoani Lindi, Salma Hamisi, amemwokoa mtoto wake Nasibu Mohamed (16) kuliwa na mamba katika Mto Sinde, alipokuwa akinawa miguu kuondoa tope.

Nasibu ambaye ni mwanafunzi katika Shule ya Msingi Sinde, kwa sasa amelazwa katika Hospitali ya Mkoa ya Sokoine, Mjini Lindi akiendelea kupata matibabu ya majeraha aliyopata kutoka kwa mnyama huyo.

Akizungumza na Nipashe aliyefika hospitalini hapo, Nasibu alisema alikumbwa na mkasa huo Machi 25, mwaka huu, majira ya saa 12:00 jioni, alipokuwa akirejea nyumbani kutokea shule.

Alisema akiwa na rafiki yake aliyemtaja kwa jina moja la Athumani, alikwenda kwenye Mto Sinde kuosha miguu kutokana na kukanyaga tope alipokuwa wanarejea nyumbani.

Alisema wakati akiendelea kunawa ndipo alipong'atwa na mamba mguu wa kushoto kisha kuanza kuvutwa kwenye maji, alipojaribu kujitetea kwa kushika tawi la mti uliokuwa jirani na mto huo hakufanikiwa.

Kwa mujibu wa mwanafunzi huyo, akiwa anapambana kujikwamua kutoka kinywaji mwa mamba huyo, alipiga kelele kuomba msaada, huku akimtuma mwenzie kwenda nyumbani kumwita babu yake.

Alisema wakati Athumani akikimbia kuelekea nyumbani, mama yake mzazi aitwaye, Salma Hamisi alimkimbilia na kupambana na mamba huyo na kufanikiwa kumwokoa.

"Nikiwa nimeshikwa na yule mamba, bahati kulikuwa na mti nikaushikilia huku nikimtuma mwenzangu akimbie nyumbani kumwita babu,"alisema Nasibu.

Alisema kabla babu yake hajafika eneo hilo mama yake alipambana kwa kumpiga na fimbo mamba huyo hadi alipomwachia.

Akizungumza na Nipashe, mama wa Nasibu, Salma Hamisi akielezea namna alivyomwokoa mtoto wake alisema akiwa anapita katika eneo hilo akitokea shambani alimsikia mtoto wake akipiga kelele za kuomba msaada na aliposogea aliona ameng'ang'aniwa mguu na mamba, ndipo alijitosa kwenye maji kupambana na mnyama huyo.

"Niliposikia kelele nilikwenda ili kujua kulikoni, ndipo nikamkuta kijana wangu akipambana na mamba nami nikajitosa kumwokoa kwa kumshika mguu," alisema Salma.

Alisema baada ya kumwokoa aliomba msaada wa pikipiki na kumfikisha Zahanati ya Mchinga alikopatiwa huduma ya kwanza na baadaye kumpeleka Hospitali ya Sokoine.

Mganga katika Hospitali ya Sokoine ambaye hakutaka kutajwa jina lake, alisema hali ya mgonjwa huyo inaimarika.

# Prof. Ngowi azikwa, wataka machapisho yake kutumika

**Na Mary Mosha,** MOSHI

ALIYEKUWA Profesa wa Uchumi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Prof. Honest Ngowi, aliyefariki dunia alizikwa juzi kijijini kwao Singa Kati, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, huku baadhi ya waombolezaji wakiomba serikali kuangalia namna ya kutumia vitabu na machapisho mbali mbali aliyowahi kuyaandika katika kukuza uchumi wa nchi.

Prof. Ngowi alipata ajali Marchi 28, mwaka huu, katika mkoa wa Pwani, iliyohusisha lori na gari ndogo Land Cruiser alilokuwa anasafiria kwenda mkoani Morogoro majira alfajiri na kukimbizwa katika Hospitali ya Rufani ya Tumbi Mkoa wa Pwani ambapo umauti ulimkuta.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake Mayagilo Dotto, alisema upo umuhimu serikali kuzikumbuka kazi zake katika kuboresha uchumi wa taifa na kuwasaidia wananchi kuacha kulalamika na kuhusu uchumi.

"Katika halmashauri na manispaa kote nchini ipo mikopo isiyo na riba, hivyo machapisho yalitolewa na wachumi kama hawa serikali iwatumie katika kuhakikisha wakinamama, vijana na watu wenye ulemavu wananufaika na kuweza kwa tija ili kukuza uchumi wa nchi yetu," alisema Dotto na kuendelea:

"Kwa sasa ipo kasumba ya vikundi kujiunga na kuchukuwa mikopo hiyo na kushindwa kurudisha, hali inayowapelekea kupata msongo wa mawazo, migogoro ya kifamilia na hata kupoteza maisha kutokana na madeni, hii ni kutokana na kukosekana elimu ya uchumi, huyu aliyatumia maisha yake yote katika kuhakikisha watu wanaupenda uchumi na kuuishi bila kujali hali za kipato na maisha yao."

Alisema umefika wakati kwa serikali kuangalia upya hali za maisha ya watu ili waweze kujijenga kiuchumi katika kupokea mifumuko ya bei bila kuchukuwa maamuzi magumu ya kujitoa uhai.

"Wapo watu wanaingia kwenye imani za kishirikina na kuwaua ndugu zao ili wapate pesa, wengine wanashiriki wizi ili kupata pesa, hii ni kukosekana kwa elimu ya uchumi, wawatumie wataalamu katika kuwawezesha kazi zao zifike kwenye jamii na kuleta matokeo chanya," alisema Dotto.

Ibada ya maziko ilifanyika katika Kanisa la Katoliki Parokia ya Kiboshi Nsinga ambapo iliongozwa na Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Dk. Charles Kitima, wakiwamo mapadri 64 wa jimbo Katoliki la Moshi na majimbo jirani ambapo alisema mchango wa wake hautasahaulika kamwe katika kanisa. "Prof. Ngowi licha ya kuwa profesa wa Chuo Kikuu Mzumbe, alikuwa ni mbobezi katika masuala ya uchumi, ameshirikiana pia na kanisa katika miradi na masuala mbalimbali yahusuyo uchumi ikiwa ni pamoja na kutoa semina mbalimbali na kuandaa maandiko mbalimbali yahusuyo uchumi wetu," alisema Dk. Kitima.

Akitoa salama za rambirambi wakati wa ibada ya mazishi mwakilishi wa Askofu wa Jimbo la Moshi Ludovick Minde, Padri Deogradius Matiika alisema Prof. Ngowi alikuwa ni msaada mkubwa kwenye shughuli mbalimbali za kanisa na maendeleo.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Eliaman Sedoyeka, alisema wao kama wizara watajitahidi kuenzi yale yote mema aliyoyaacha kwa vitendo.

"Kwa kushirikiana na wachumi wengine waliopo nchini tutaendelea kuhamasisha wanafunzi kupenda uchumi kwanzia ngazi za msingi, tutawatumia wataalamu kuleta mabadiliko ya kifikra katika uchumi wetu wa sasa na baadaye," alisema.

Nao baadhi ya majirani waliohudhulia maziko hayo, akiwamo Sabastiani Mallya (79), alisema hashangai kuona umati mkubwa wa watu umefika kumsindikiza Profesa huyo kutokana na hali yake ya upendo kwa jamii.

"Alikuwa akija nyumbani wazee wote wa hapa tunamshukuru Mungu kwani atakuja kututembelea na kuleta posho ya tumboni, amejitahidi kuhakikisha vijana wengi wa hapa mtaani wamesoma kwa kuwatafutia wafadhili mbalimbali hadi wengine wamekuwa mapadri na wengine wana maisha wanaishi huko mjini," alisema Mallya.

## Jeshi la Polisi latoa ufafanuzi trafiki kupiga tochi kwa kificho

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani limetoa ufafanuzi kuhusu matumizi ya 'tochi' kwa askari wa usalama barabarani kwa kueleza kwamba Sheria ya Usalama Barabarani inamruhusu askari kusimama eneo lolote kwa ajili ya kuchukua picha ya magari yanayoenda kwa mwendo kasi.

Kamanda wa kikosi hicho, Wilbroad Mtafungwa aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akijibu maswali kutoka kwa waandishi wa habari kuhusu malalamiko yanayotolewa na madereva dhidi ya askari wanaowapiga tochi wakiwa mwendo wa kasi barabarani wakiwa wamejificha.

Mtafungwa alisema hakuna sheria inayomkataza askari wa usalama barabarani kusimama eneo lolote kuchukua picha kwa kutumia 'Speed Radar' na wanafanya hivyo ili kuwabaini wanaokiuka sheria na kuhatarisha maisha ya watu.

Alisema madereva wanapaswa kufuata sheria inavyoelekeza ili kuepuka kukutana na mkono wa sheria na siyo kutaka kuwapangia askari eneo la kuwapiga tochi. "Hakuna kuonewa kama madereva wa vyombo vya moto wanavyodai. Askari anavizia ili apate picha bora itakayomwezesha kuona kosa lililofanywa na dereva,"alisema Mtafungwa.

Alisema Jeshi la Polisi litatoa elimu kwa madereva na makundi mbalimbali wanaotumia vyombo vya moto ili kujua sheria hiyo.

Kadhalika alikemea vitendo vya rushwa kwa baadhi ya askari wa barabarani kwa kueleza kuwa suala hilo linashughulikiwa kikamilifu Makao Makuu ya Kikosi cha Usalama Barabarani pamoja na makamanda wa polisi wa usalama barabarani mkoa na wilaya. Kamanda Mutafungwa alisema hakuna sheria inayomruhusu askari kuchukua rushwa kwa madereva wanaofanya makosa barabarani. Hivyo, alliwataka wananchi kutokuwa na wasiwasi kuhusiana na sheria za barabarani, huku akiwasisitiza madereva na jamii kuwa makini na sheria zilizowekwa za barabarani ili waepuke kukutwa na makosa.


**GARI ZINAUZWA**

MAZDA CX7 SPECIAL EDITION (NYEUSI)4WD 2,300 c.c PETROLI IPO KATIKA HALI NZURI.IMETEMBEA 65,000km,TOYOTA CAMI (NYEUSI) 4WD 1,300 c.c PETROLI IPO KATIKA HALI NZURI IMETEMBEA 115,000km

**KWA MAWASILIANO NAMBARI:0737 708 890/0755 378 346**


**KUPOTEA KWA PASSPORT**



CHARLES SAMSON KABEYA anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria (Passport) yenye namba **AB 557567.** Kwa yeyote atakaye iona atoe taarifa Kituo chochote cha polisi . POLISI TAARIFA:

RB NO.MZN/6856/2021.

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
MATRIMONIAL CAUSE NO 4 OF 2022
HILDEGALDA
NGONGOKI.........................PETITIONER
VERSUS
JEROME KILASARA
KIWIA.........................RESPONDENT
TO: JEROME KILASARA KIWIA
MAILI MBILI DODOMA
**0762745963/ 0682597456/0657687026**

**NOTICE OF DATE OF MENTION**

THE NOTICE that the above case has been fixed for MENTION on **20th day of April 2022 at 9:00am** Before Honourable Mpelembwa S.RM.
YOU ARE required to appear in this District Court Without fail and you must produce on that day all documents upon which you intend to rely in support of your case.
GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT

This 1st day of April 2022

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA

## TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA

### TAARIFA YA UPANUZI WA MASHIMO YA GENA NA GOKONA YALIYO KATIKA MGODI WA DHAHABU WA NORTH MARA, WILAYA YA TARIME, MKOA WA MARA

Mradi pendekezwa wa upanuzi wa mashimo ya Gena na Gokona (Mradi) upo ndani ya Wilaya ya Tarime katika Mkoa wa Mara nchini Tanzania. Mradi pendekezwa unamilikiwa na Mgodi wa Dhahabu wa North Mara (NMGM) ambayo ni kampuni ya utafutaji na uchimbaji madini inayomilikiwa na kampuni ya Twiga Corporation, iliyoundwa kwa ubia kati ya Barrick (84%) na Serikali ya Tanzania kwa (16%). Eneo la Mradi liko chini ya Leseni ya Uchimbaji Maalum (SML 17/96). Mradi pendekezwa unazigusa kata nne ambazo ni Nyamwaga, Nyarokoba, Kibasuka na Kemambo pamoja na sehemu za vijiji vitano: Komarera, Genkuru, Msege, Kewanja na Nyakunguru.

Upanuzi wa mashimo ya Gena na Gokona ni muendelezo wa shughuli za uchimbaji pamoja na faida za kiuchumi zitokanazo na shughuli hizo za uchimbaji. Kwa miaka mingi, NMGM imekua ikiendeleza tafiti katika eneo hilo ambazo zimeonyesha uwepo wa mashapo yaliyopo kwenye mashimo hayo.

Ili kutekeleza Mradi pendekezwa, Tathmini ya Athari za Mazingira (TAM) itafanyika kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, Kanuni za Tathmini ya Athari za Mazingira ya mwaka 2005 na marekebisho yake ya mwaka 2018 pamoja na Sheria ya Madini ya mwaka 2010.

NMGM imeziteua kampuni za Digby Wells Environmental na PAULSAM Geo-Engineering Limited kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM). Utafiti huo utachunguza athari chanya na hasi kwenye mazingira na jamii zitakazotumika kuunda Mpango wa Usimamizi wa Mazingira kwenye utekelezaji wa Mradi.

Kwa kuzingatia utaratibu, usajili pamoja na uwasilishwaji wa taarifa za awali za mradi kwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) unaendelea kama sehemu ya TAM. Tangazo hili linawakaribisha watu wote wenye nia, ushauri au maarifa kuhusu athari zozote ama za kimazingira au kijamii zinazohusiana na mradi huu kuwasilisha mawazo yao kwa kupitia anuani zifuatazo:

| Mdhibiti | Muwekezaji | Wataalamu washauri elekezi |
|---|---|---|
| Mkurugenzi Mkuu<br>Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC),<br>S.L.P. 63154, Regent Estate,<br>Dar es Salaam, Tanzania.<br>Simu: +255 22 2774889<br>Barua pepe: dg@nemc.or.tz | Mgodi wa Dhahabu wa North Mara (NMGM)S.L.P. 422<br>Tarime<br>Tanzania<br>Faksi: 255282621903<br>barua pepe: apolinary.lyambiko@barrick.com | PAULSAM Geo-Engineering Company Limited,<br>Ghorofa ya 07 , Faykat Tower Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Dar es Salaam, Tanzania.<br>S.L.P. 70812<br>Simu/Faksi: +255 755561188<br>Barua pepe: piliseleman@gmail.com<br><br>ESD Advisory Ltd T/A Digby Environmental<br>Madai Crescent, Plot 151, Ada Estate, Dar es Salaam.<br>Jamii:+255717087482<br>Barua pepe: Deogratius.lorri@digbywells.com |

**Ushirikishwaji wa wadau utafanyika kama sehemu ya mchakato wa TAM ambapo habari zaidi zinazohusiana na mradi zitawasilishwa.**

216778302



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (kushoto), akisalimiana na Mkuu wa Kitengo cha Biashara za Serikali wa Benki ya NMB, Vicky Bishubo (katikati), baada ya kuuwasha rasmi Mwenge wa Uhuru mkoani Njombe ambapo alikuwa mgeni rasmi. Kulia ni Spika mstaafu, Anna Makinda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mawaziri waelekeza utatuzi migogoro ya ardhi vijiji 975

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ametaka elimu na ushirikishwaji wananchi kupewa kipaumbele wakati wa utekelezaji maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975.

Alitoa kauli hiyo mkoani Tanga juzi wakati yeye na timu yake ya Mawaziri wa Wizara za Kisekta wakitoa mrejesho wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri kwa viongozi wa mkoa na wilaya katika mkoa huo kuhusiana na migogoro ya matumizi ya ardhi.

Katika maamuzi yake, Baraza la Mawaziri lilipendekeza vijiji 14 katika mkoa wa Tanga kubaki maeneo ya hifadhi na kufanyiwa marejebisho ya mipaka, huku vijiji viwili na mitaa miwili kufanyiwa tathmni kutokana na sehemu kubwa ya maeneo yake kuwa na umuhimu kwa maslahi ya Taifa.

Katika mkoa wa Tanga maeneo yenye mgogoro wa matumizi ya ardhi yanahusisha wananchi na Hifadhi ya Msitu wa Mikoko na Shamba la Taasisi ya Utafiti wa Mifugo katika Kituo cha TALIRI.

Maeneo mengine ni kwenye Hifadhi za Misitu Chang'andu, Kwani na Gendagenda pamoja na mgogoro katika Pori Tengefu la Mto Umba na ule wa Shamba la Mwele-ASA.

"Rai yangu katika utekelezaji maamuzi haya ya Baraza la Mawaziri ni ushirikishwaji ili asitokee mtu akalalamika kaonewa au kafanyaje, jukumu letu kama serikali ni kuhakikisha tunatoa elimu pia ili masuala haya yasijirudie kwa sababu tumekuwa na operesheni mbalimbali ambazo mwisho wa siku utekelezaji au usimamizi wake ubakuwa siyo mzuri sana," alisema na kuongeza:

"Kipindi hiki Rais Samia asingependa kuona masuala haya ya migogoro ya matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali yanajirudia ndiyo maana katika Wizara ya Ardhi imetoa fedha nyingi ili kumalizana na migogoro ya ardhi."

Alisisitiza suala la uwajibikaji kwa watendaji wa serikali kuanzia mkoa hadi kijiji na kuwataka kila mmoja kusimamia majukumu yake ili masuala ya uvamizi kwenye hifadhi na taasisi za umma yasijirudie.

"Tunaporekebisha maeneo haya hatutarajii tena uvunjifu wa sheria uendelee uongozi kuanzia ngazi ya kijiji muwe walinzi wazuri wa maeneo hayo ili kuepuka migogoro hiyo ya wananchi kujimegea maeneo ambayo siyo rasmi kwa makazi," alisema Dk. Mabula.

Mawaziri walioko kwenye ziara hiyo mkoani Tanga walielezea hatua na mikakati ya kuchukua wakati wa utekelezaji maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusiana na utatuzi wa migogoro katika vijiji 975.

Naibu Waziri wa Uvuvi na Mifugo, Abdallah Ulega, alisisitiza suala la watendaji wa serikali kuwa imara wakati wa kusimamia zoezi zima la utekelezaji maamuzi hayo ili kuepuka kupata tabu kwenye utekelezaji.

Kwa upande wake Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Hamis Chillo, aliwahimiza watendaji wa serikali kuhakikisha wanasimamia na kutunza mazingira hususan kwenye maeneo ya vyanzo vya maji na kusisitiza utumiaji busara wakati wa utekelezaji maamuzi ya Baraza la Mawaziri.

Anthony Mavunde, Naibu Waziri wa Kilimo, alielezea mikakati ya serikali kupitia wizara yake katika kujikita kwenye uzalishaji mbegu ili kukidhi mahitaji ya nchi na kuepuka uagizaji mbegu kutoka nje ya nchi sambamba na kufanya utafiti katika mashamba yake yaliyovamiwa.

Dk. Mabula ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri wa Kisekta, aliwaasa wananchi hasa waliotengewa maeneo yaliyowekewa mipango ya matumizi ya ardhi kuwa, serikali haitarajii kuona tena wakiingia maeneo ya hifadhi na vyanzo vya maji yaliyozuiliwa kwa kuwa uvamizi uliofanywa ndiyo uliosababisha migogoro ya matumizi ya ardhi.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, wizara yake isingependa kuona mambo haya yanajirudia na wale wote ambao mara nyingi wanavamia maeneo na kutarajia serikali kuridhia kuendelea wawepo maeneo hayo, suala hili halitajirudia tena na kinachotakiwa sasa kila mmoja atekeleze wajibu wake kwa kutii sheria bila shuruti kwani serikali haiwezi kuwa na mazoezi haya kila mwaka.

## Ujangili wa kitoweo, shughuli za kijamii tishio kwa uhifadhi

**Na Salome Kitomari**

UJANGILI wa kitoweo, mimea vamizi, shughuli za kibinadamu na kuongezeka kwa migogoro kati ya binadamu na wanyama kumeongeza changamoto kwa Hifadhi ya Jamii ya Burunge (Wildlife Management Area (WMA), iliyopo wilayani Babati mkoani Manyara.

Hifadhi hiyo imeathiriwa na janga la UVIKO-19 kutokana na watalii wanaotembelea eneo hilo kupungua, huku maeneo ya uwekezaji yakikosa wageni kabisa, hali iliyoporomosha mapato kutoka Sh. bilioni 2.2 mwaka 2019/20 hadi chini ya milioni 400 mwaka jana.

Hayo yalibainika hivi karibuni wakati wa ziara ya waandishi wa habari wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), waliotembelea eneo la Burunge WMA kupitia mradi wa Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID Tuhifadhi Maliasili).

Katibu wa Burunge WMA, Benson Mwaise, alisema changamoto iliyopo ni wenyeji kuingia hifadhini kwa ajili ya kuwinda kitoweo huku wengine wakiuza kwa wengine, na kwamba wanaikabili kwa kuendelea kuemilisha wananchi umuhimu wa kutunza raslimali hiyo.

Alitaja idadi ya kesi za ujangili kwa kipindi cha miaka sita ambazo ni mwaka 2016 (4), 2017 (14), 2018 (4), 2019 (8), 2020 (1) na 2021 (8), kwa kushirikiana na mamlaka nyingine zinazoendelea kwenye Mahakama mbalimbali.

Aidha, nyingine ni ongezeko la watu kwenye vijiji ambao hutumia maeneo ya mapori ambayo walikuwa hawayatumii yalikuwa yanatumiwa na wanyama, lakini sasa wamefungua mashamba hadi kwenye mipaka, huku wanyama wakiwa hawana mipaka bali huvuka na kwenda kula mazao au kukaa hifadhini na kula mazao.

"Ukiwa kwenye moja ya kilimo cha WMA utaona jinsi mashamba yanazidi kufunguliwa kiasi kwamba eneo la uhifadhi limebaki ndilo lenye mapori, hii imeongeza changamoto ya migogoro ya wanyama na binadamu, kila siku kuna malalamiko ya wanyama kuharibu mazao, ukiangalia ni kwamba watu wanalipa hadi kwenye mpaka wa hifadhi," alisema.

"Tunatoa elimu ya uhifadhi na uzazi wa mpango, watu wanazaliana kwa wingi tumeamua kutoa elimu ya uzazi kwa wananchi wetu, pia namna ya kufuga kisasa kuacha kuwa na mifugo mingi ambayo haina tija."

"Nyingine ni kujifunga kwa shoroba ya Kwakuchinja, unakuta kijiji kiliacha eneo fulani kama pori au msitu wao lakini sasa wamefungua mashamba, wanyama walishazoea kupita au kukaa huko wanasumbuliwa au wanaingia kwenye mgogoro na binadamu,"alisema.

Nyingine ni kuongezeka kwa mimea vamizi ambayo inaharibu uoto wa asili kiasi cha kuwafanya wanyamapori na wafugwao kukosa malisho, na kwamba kila kukicha maeneo yanapungua na ndiyo maana migogoro haiishi.

Kuhusu ushiriki wa wanawake, alisema kwenye vijiji kuna vikundi vya wanawake wanaofanya ujasiriamali wa kukabiliana na changamoto za maisha, huku kwenye Baraza la WMA kati ya wajumbe 30 wanawake ni watano.

Naye Makamu Mwenyekiti wa WMA, Naserin Mollel, alisema wanaelimisha jamii hiyo kuwaamini wanawake na kuwashirikisha kwenye majukumu mbalimbali, huku wakieleza changamoto ni jamii hiyo kuamiani wanaweza kufanyakazi za ulinzi au kwenda kufukuza wanyama hasa nyakati za usiku.

Aidha, alisema kuna changamoto kubwa ya uchafuzi wa mazingira kwa magari yanayopita kwenye barabara ya Arusha -Babati ambayo inapita eneo la hifadhi na shoroba hiyo, na kwamba kwa kipindi cha miezi mitatu walikusanya takataka tani saba kati eneo la ukubwa wa kilomita saba.

WMA hiyo yenye kilomita za mraba 283 inamilikiwa na vijiji 10 vya Mwada, Sangaiwe, Ngolley, Vilima Vitatu, Kakoi, Minjingu, Olasiti, Maweni, Magara na Manyara ambavyo vinawajibika kutunza eneo hilo.

# Profesa Ngowi alivyofanya mambo magumu kuwa mepesi

**Na Jenifer Gilla**

KATIKA uhai wake aliyekuwa Mhadhiri wa Uchumi katika Chuo Kikuu Mzumbe, Prof. Honest Ngowi, hakuishia tu kutoa elimu vyuoni bali kwa wananchi wa kawaida mtaani.

Katika kuhakikisha kuwa jamii inanufaika na talanta ya uchumi aliyojaaliwa aliandaa vipindi vya mafunzo mbalimbali na kuviweka katika Channel yake inayoitwa Ngowi TV.

Leo tunaangazia moja ya masomo yake aliyoyatoa kwa wajasiriamali wa soko la Kariakoo 'Jinsi ya kujitofautisha kibiashara'.

Prof. Ngowi anaanza kwa kusema kuwa ni muhimu kujitofautisha kibiashara kwa sababu haupo mwenyewe kwenye tasnia.

"Tunasema biashara zipo zaidi ya 1,000, wewe kama una duka kuna maduka zaidi ya mia moja mbele ya hilo duka lako, kama una mgahawa kuna mingine 3,000 mbele yako, suala la msingi wewe unakuwa tofauti vipi na wengine ili uweze kumvutia mteja," alisema.

Alisema katika biashara kuna mambo mawili muhimu, kumvuta mteja na kumbakiza, na kwamba kumvuta ni jambo rahisi lakini kumbakiza ni jambo gumu na kitakachomtofautisha na wengine ni namna atakavyotoa huduma bora kwake.

Alisema jambo la kwanza la kujitofautisha ni namna utavyomjali mteja, kuanzia anapokuja katika biashara yako hadi anapoondoka, ikiwamo kauli na huduma ya haraka.

Jambo lingine alitaja kuwa ni mazingira ya eneo la biashara, akitolea mfano wa mapambo, muziki na usafi, mteja atavutiwa kulingana na hayo mambo akitolea mfano wa kama mgahawa utapigwa nyimbo za dini basi watavutiwa wateja wanaopenda nyimbo hizo.

Jambo lingine alisema ni kutoa huduma ya bure kwa wateja wanaokuja katika ofisi yako, akitolea mfano kwa madereva tax kuweka huduma ya WIFI ya bure kwa wateja. Alisema huduma hii inatumika sana nchi za nje ikiwamo Marekani na Nigeria lakini Tanzania bado haijafika. Mchumi huyo alisema pia lazima kuacha kazi ya mawasiliano pale unaagana na mteja wako hasa kwa madereva taksi kwamba inasaidia mteja kukutafuta pindi atakapokuja tena mahali hapo.

Kwa wafanyabiashara wa mboga, matunda na vyakula sokoni, Prof. Ngowi alisema wanaweza kujitofautisha na wengine kupitia kuweka bidhaa zao kwenye vifungashio na kufurahia kuwa wafanyabiashara wengi wa bidhaa hizo wanatumia mbinu hiyo.

Kwa wakulima anashauri wajitofautishe kwa kujikita kwenye kilimo hai kisichotumia kemikali ingawa gharama zake ni za juu ukilinganisha na cha kisasa.

Prof. Ngowi alisema kuna watu wapo tayari kutoa pesa zaidi ili kupata mboga ambazo hazina kemikali na dawa.

Alishauri pia wakulima kulitafuta soko ikiwamo kutengeneza vipeperushi vinavyohusu bidhaa wanazouza pamoja na mawasiliano yao na kuzisambaza kwa wateja, ikiwamo maduka makubwa ya vyakula (supermarkets), ili iwe rahisi kuteka soko na kuepuka kukaa na bidhaa muda mrefu hadi kuharibika.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara kufanya utafiti wa masoko kwenye eneo analokwenda kuanzisha biashara ili kujua ni kitu gani mwenzake hana naye awe nacho.



Mwenyekiti wa Taasisi ya Sululu Foundation, Aisha Sululu (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mashindano ya kitaifa ya kusoma Qur'an yatakayofanyika Aprili 10 katika viwanja vya Mnazi Mmoja. Kulia ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Al- Hikma, Sheikh, Nurdin Kishik. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# EWURA yaeleza mwenendo wa hali ya mafuta

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) imesema inatarajia bei ya mafuta itaendelea kupanda kutokana na uhitaji wake kuwa mkubwa, huku usafirishaji na upokeaji wake nchini ukiwa ni hafifu kwa sababu ya vita inayoendelea kati ya Russia na Ukraine.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo, Godfrey Chibulunje, wakati wa mdahalo uliohusisha waharIri wa waandishi wa habari, alisema mfumuko wa bei pia unasababishwa na changamoto inayoikumba miundombinu ya usafirishaji kutokana na sababu mbalimbali za kivita.

Alisema bei za mafuta katika soko la dunia zimebadilika kwa kiasi kikubwa, akieleza kuwa mwezi Desemba 2021 tani moja ya mafuta ya petroli yalikuwa yanauzwa dola 717 na hadi kufika Machi mwaka huu ilipanda hadi kifikia dola 1,106 kwa tani moja.

"Bei za mafuta zinatofautiana sana katika maeneo mbalimbali duniani, barani Afrika, Ulaya na America, wakati Tanzania lita moja ya dizeli ikiwa inauzwa Sh. 2403, Kenya ni 2,331 na Uganda 2,830, kwa hiyo ukiangalia nchini kulikuwa na unafuu kwa kiasi fulani," alisema.

Aliongeza kuwa kesho watatangaza bei mpya ya mafuta, akieleza kuwa baada ya matukio ya vita kuisha hali itarudi kuwa ya kawaida, huku akiwataka Watanzania kujiwekea utaratibu mzuri katika matumizi ya bidhaa hiyo, akisisitiza kuwa mamlaka hiyo itaendelea kusimamia mwenendo wa uuzwaji wa mafuta nchini.

Aidha, alieleza kuwa hali inazidi kubadilika hivyo alitoa wito kwa watanzania kuangalia njia m'badala za kuhakikisha wanaendelea kuendesha shuhuli za kiuchumi na hata kuanza kufikiria kutumia magari yanayotumia gesi na umeme kama mbadala wa mafuta.

Alisema serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya upokeaji wa mafuta bandarini ili kutatua changamoto ambazo ziko ndani ya uwezo wake.

# Afrika yatakiwa kuongeza jitihada za kutunza misitu

**Na Salome Kitomari**

JUKWAA la Misitu Afrika (AFF), limesema kuwa bado zinahitajika jitihada za makusudi kutunza misitu ili iwe endelevu kwa kizazi cha sasa na kijacho, kwa nchi kuwa na mipango inayotekelezeka kupitia sera, sheria na usimamizi wa utekelezaji wa mikataba na makubaliano ya kimataifa.

Hayo yalibainishwa hivi karibuni na wadau hao waliokutana Mombasa nchini Kenya, kwenye semina ya kushirikishana uzoefu na taarifa kuhusu changamoto na fursa zilizoko kwenye utunzaji na uhifadhi endelevu wa misitu katika wakati wa mabadiliko ya tabia nchi.

Katibu Mtendaji wa AFF, Prof. Godwin Kowero, alisema mkutano huo uliokutanisha wadau kutoka nchi mbalimbali za Afrika, walijadiliana mabadiliko ya tabianchi namna ya kuboresha usimamizi wa misitu, matumizi ya ardhi na rasilimali misitu barani humo.

"Tumeangaliana jinsi nchi za Afrika zilivyopokea na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwenye misitu, zinavyotekeleza mkataba wa Paris hasa kwenye usimamizi wa misitu, sera na mipango kuhusu mabadiliko ya tabianchi, uwezo na utekelezaji wa shughuli za MKUHUMI+ unavyoweza kuboreshwa kwenye nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara," alisema.

Aidha, alisema walibaini bado kuna changamoto kubwa ya utekelezaji wa sera na sheria kwa kuwa zipo ambazo ni nzuri, lakini hazitatekelezwa ipasavyo, huku changamoto za utunzaji wa rasilimali hizo kwa muundo endelevu zikiongezeka.

Mengine ni kifuatilia matumizi ya raslimali na bidhaa mbalimbali kama gundi ambazo zinaweza kufanywa na wajasiriamali katika kuimarisha maisha, ajira, kupata kipato chao na taifa kwa ujumla huku misitu ikiendelea kutunzwa.

"Utafiti mwingine ni umuhimu wa kupunguza nishati ya mafuta barani, ili kukabili ongezeko la joto duniani kwa kuangalia uwezekano wa kuzalisha na kutumia nishati ya mimea kwa muktadha wa kukuza uchumi," alisema.

Alisema pamoja na kuboresha utawala wa ardhi na misitu barani wamefanya utafiti wa kuelewa bora wa sera na mazoea ya usimamizi wa rasiliamali hizo Afrika.

Pia aliangalia mabadiliko ya vichocheo muhimu vinavyohusika na upotevu wa misitu barani Afrika na jinsi nchi zinavyoweza kupanga shughuli za misitu kwa usimamizi na mipango ya raslimali hiyo muhimu kwa maendeleo ya watu.

Alisema tangu kuanzishwa wa AFF mwaka 2007 imejishughulisha na mipango mbalimbali ya PanAfrika ya namna ya miti na misitu inavyosaidia ustawi wa maisha barani, kipato cha wananchi na mazingira tunayoishi. "Kwa AFF, watu na mazingira yao ni eneo letu la kipaumbele. Misitu na miti nje ya misitu ni raslimali ambayo lazima kuitunza iwe endelevu na ndiyo maana tumekuwa mstari wa mbele kueleza umuhimu wa watu kuboresha mazingira wanayoishi kwa kutunza ardhi na misitu," alisema.

Alisema tafiti kadhaa na mipango imefanywa na AFF kwa kushirikiana na wadu mbalimbali kwa kuwa na mikutano ya kujadili na kutoka na maazimio ambayo huzishauri serikali za Afrika na wadau juu ya hatua madhubuti za kuchukua katika kutunza misitu.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Lala salama Ligi Kuu, TFF ikisinzia tutavurunda CAF*

**LIGI** Kuu Bara imeingia raundi ya 19, ambapo mzunguko huu utakapokamilika kila timu itakuwa imebakiza mechi 11 kabla ya kumalizika kwa msimu huu wa 2012/22 ambao unashirikisha timu 16, mbili za mkiani zikishuka daraja moja kwa moja kwenda kucheza Ligi ya Championship msimu ujao.

Lakini, timu mbili zitakazoshika nafasi ya 13 na 14, zitacheza mechi ya mchujo dhidi ya timu mbili zitakazoshika nafasi ya tatu na ya nne kwenye Ligi ya Championship kuwania nafasi mbili za kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

Hadi ligi hiyo inarejea juzi baada ya kumalizika kwa Kalenda ya Fifa, Yanga bado ndiyo ipo kileleni mwa msimamo ikiwa na alama 48, huku ikifuatiwa na Simba yenye pointi 37 katika nafasi ya pili na hali ikiwa mbaya zaidi kwa Tanzania Prisons inayoburuza mkia ikiwa na pointi 13, moja nyuma ya Mbeya Kwanza iliyopo nafasi ya 15.

Kwa ujumla msimu huu umekuwa na ushindani mkubwa zaidi ndani ya muongo mmoja sasa, hivyo katika raundi kama hii Shirikisho la Soka nchini (TFF), likishirikiana na Bodi ya Ligi (TPLB), kwa kuvishirikisha vyombo vya usalama na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), hawana budi kuzidi kuimulika ligi hiyo kwa umakini zaidi ili kuepuka kupata bingwa asiyestahili.

Tunatambua mbali ya timu zilizopo katika mbio ya ubingwa, lakini pia zipo zinazohaha kujinasua katika mstari wa kushuka daraja, kucheza mechi za mchujo na zinazotaka kumaliza nafasi nne za juu ili kunufaika na bonasi kubwa kutoka kwa wadhamini, hivyo ni kipindi ambacho umakini zaidi unahitajika kwa kuanza kuwamulika viongozi wa klabu, wachezaji hadi waamuzi.

Ikumbukwe kwa mujibu wa mkataba ambao TFF iliingia na Kampuni ya Azam Media Limited Mei mwaka jana kwa upande wa haki za matangazo ya televisheni ambao una thamani ya Sh. bilioni 225.6 kwa kipindi cha miaka 10, kuna bonasi kubwa mwishoni mwa msimu kutegemea na nafasi timu itakayomaliza kuanzia bingwa hadi itakayoburuza mkia.

Kwa bingwa, mbali na kombe na zawadi kutoka kwa Mdhamini Mkuu, Benki ya NBC, Azam Media Limited itatoa bonasi ya Sh. milioni 500, mshindi wa pili milioni 250, watatu milioni 225, wa nne milioni 200 na zitakwenda zikipungua hadi mwisho na zitakazocheza mechi ya mtoano zikilamba milioni 20 kila moja.

Hivyo, raundi hii kunahitajika umakini mkubwa kwani timu zote zinauhitaji mkubwa wa kumaliza nafasi za juu ili kupata bonasi kubwa, lakini fedha zinazopata zinaweza kutumika vibaya katika kutafuta matokeo nje ya uwanja kwa kutembeza rushwa ili kupanga matokeo.

Kwa kuwa bingwa huiwakilisha nchini kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tunachotaka kukiona sisi ni ligi hiyo ikimalizika kwa kupatikana bingwa aliyestahili ili mwakani aweze kuipeperusha vema bendera ya Tanzania katika michuano hiyo ya kimataifa ya kwanza kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Lakini kama Simba ambayo jana usiku ilikuwa ikicheza dhidi ya US Gendarmerie ya Niger kwenye mechi ya hatua mwisho ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, ikihitaji kushinda ili kutinga robo fainali, endapo imefanikiwa kusonga mbele kuna uwezekano mkubwa wa kuingiza timu nne kwenye michuano ijayo ya kimataifa; mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho.

Kwa mantiki hiyo, ni wazi timu tatu zitakazomaliza nafasi ya juu, zinaweza kupata tiketi ya kuiwakilisha nchini kwenye michuano ya kimataifa msimu ujao, jambo ambalo tunataka kuona umakini mkubwa unafanyika katika ligi hiyo ili kutoa wawakilishi waliostahili na si wakiujanjaujanja.

Lengo letu ni kuona kama Tanzania itafanikiwa kuingiza timu nne kwenye michuano hiyo ya CAF msimu ujao, basi zote zifike hatua ya makundi robo fainali na kuendelea, na si kuishia raundi ya awali kama ambavyo imetokea msimu huu kwenye michuano hiyo inayoendelea Afrika.

Aidha, tunataka kuona Tanzania ikiwa nchi ambayo kila msimu inaingiza timu nne kwenye michuano hiyo ya CAF, lakini hilo litawezekana tu kama wawakilishi watakaopatikana angalau watakuwa wanajitutumua hatua ya makundi, robo fainali na kuendelea, kwa kuwa katika hatua hizo ndiyo nchi husika hupata pointi nyingi, hivyo bila TFFna TPBL kumulika kwa umakini mechi hizi 11 zilizosalia itakuwa ndoto hilo kutokea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Rundo la majeruhi Simba, Yanga linafikirisha

**KLABU** kongwe nchini Simba na Yanga ndizo timu zenye majeruhi wengi sana kwenye vikosi vyao mpaka sasa. Kwa namna moja ama nyingine zimekuwa vikiathiri pia mwenendo wa timu zao kwenye Ligi Kuu na Kombe la FA na timu ya Simba imekuwa ikiathirika zaidi kwenye baadhi ya mechi zake za kimataifa.

Simba imekuwa na baadhi ya majeruhi ambao wakishaumia kupona inakuwa mtihani, wengine wakiumia mara kwa mara, kikubwa zaidi wakati mwingine wanakuwa wengi kwa wakati mmoja.

Mfano kama Chris Mugalu amekuwa ni majeruhi wa kudumu. Amekuwa kwenye chumba cha daktari zaidi badala ya uwanjani, kwani akicheza mechi mbili au tatu, basi ataumia na kurejea kwake inaweza kupita mechi sita, nane au kumi, ndipo arejee tena.

Majeruhi wengine wa mara kwa mara ni John Bocco, Thadeo Lwanga yeye aliumia na kukaa kwa muda mrefu, Mzamiru Yassin, huku mchezaji tegemeo kwa sasa Pape Sakho yeye amekuwa akiumia mara kwa mara, lakini akirejea kwa muda mfupi, tofauti na mwanzoni aliposajiliwa, na kuumia kwenye mechi za kwanza na akakaa kwa muda kidogo bila kucheza.

Kwa upande wa Yanga, kuna Kibwana Shomari, Abdallah Saibu 'Ninja', Feisal Salum 'Fei Toto', Yacouba Songne, ambaye tayari sasa ameanza mazoezi baada ya kukaa nje kwa muda mrefu, Yassin Mustapha. Pia hata Djuma Shaaban. Mwingine ambaye ni majeruhi wa mara kwa mara ni Khalid Aucho.

Hivi karibuni Fei Toto aligundulika kuwa ni majeruhi kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars, lakini akiwa anacheza kwenye timu yake ya Yanga.

Kama ni kweli, Fei Toto alikuwa anacheza kwenye timu yake ya Yanga akiwa ni majeruhi, basi ni jambo la hatari ambalo linaweza kumfanya awe majeruhi wa kudumu, lakini linaweza kufupisha karia yake ya soka, akiwa bado na umri unamruhusu kucheza.

Tuliona wachezaji wa zamani waliokuwa wakipigwa sindano za ganzi ili kuendelea kuzitumikia timu zao wakati wakiwa majeruhi mwisho wao wa soka haukuwa mzuri.

Na klabu zilizokuwa zikifanya hivyo, ziliwaacha na kutafuta wachezaji wengine, maisha yakaendelea.

Tukirudi kwenye mada yetu kuu, ni kwamba inawezekana kweli wachezaji wa klabu za Simba na Yanga ndiyo wanaowindwa sana na timu zingine ili kuumizwa.

Cha ajabu ni kwamba baadhi ya wachezaji wa timu hizo hizo huwa hawaumii kihivyo. Hata kama wataumizwa, basi watapata matibabu na kupona kwa muda mfupi.

Wachezaji kama Meddie Kagere, Clatous Chama, Mohamed Hussein, na wengineo hata Luis Miquissone ambaye ameondoka klabu ya Simba, ni aghalabu sana kutokea kuumizwa na kukaa nje sana, licha ya kupaniwa na wapinzani.

Fiston Mayele, Yanick Bangala, Bakari Mwamnyeto, Deus Kaseke na wengineo wa Yanga ni wachezaji sugu ambao huwezi kukuta wakiumia mara kwa mara.

Hapo ndipo tunajiuliza, tatizo ni wachezaji wenyewe wanakuja wakiwa na majeraha ya kudumu ila klabu zetu zinashindwa kuwachunguza vya kutosha, au vitengo vya tiba vya klabu za Tanzania vina matatizo?

Mimi nadhani klabu hizi zianze kuwafanyia uchunguzi wa kina wachezaji wa nje na wa ndani ambao inataka kuwasajili, badala ya kuwa na mihemko tu ya kumhitaji mchezaji fulani kuogopa atachukuliwa na timu nyingine, hivyo kuwahi kumsajili.

Wengine wanakuwa na majeraha ya kudumu, hivyo baadaye kuzigharimu timu, kwa kupata mishahara ya bure huku wakikaa muda mrefu bila kucheza.

Huwezi kukuta kitu kama hicho Azam FC, pamoja na matatizo waliyonayo, lakini kwenye suala la kuchunguza afya za wachezaji wapo vizuri. Hawachunguzi kwa fasheni. Ndiyo maana imekuwa ni timu iliyowapeleka wachezaji wengi nje ya nchi kuwatibia.

Wachezaji nao wana tabia ya kudanganya umri, hivyo vitengo vya tiba huwapatia dawa kulingana na umri walioutaja, hivyo kusababisha wasipone upesi wanapokuwa na majeraha.

Ni wakati sasa wa klabu kuimarisha vitengo vyao vya tiba ili kutoingizwa mkenge na baadhi ya wachezaji wenye majeraha ya kudumu ambao wanaonekana kama wanakuja kujiunga na timu za Tanzania kama sehemu ya kupumzika tu na kupiga hela si kucheza soka.

# Chana alivyoingia kwa kasi Maliasili na Utalii

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, ameahidi kushirikiana na watendaji na watumishi wa wizara yake katika kutekeleza majukumu mbalimbali.

Alielezea mwelekeo wake katika wizara yake mpya baada ya kuapishwa na Rais Samia Suluhu Hassan jijini Dodoma juzi.

Kauli hiyo aliitoa alipowasili katika ofisi za Wizara ya Maliasili na Utalii zilizoko Mtumba jijini Dodoma.

"Niwahakikishie kwamba niko tayari kuchapa kazi pamoja nanyi, imani kubwa ambayo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ametupa hatutamwangusha," alisema Chana.

Aidha, aliweka bayana kuwa yuko tayari kufanya kazi kwa saa 24 bila kikwazo chochote.

"Mimi waziri wenu milango iko wazi saa 24, hakuna wakati sitapatikana iwe ni usiku, iwe asubuhi hata iwe sikukuu na ndio maana ya kuwa mtumishi wa umma," alisisitiza.

Naye Waziri wa Katiba na Sheria, aliyehamishwa kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, alisema kuwa wizara imepata mtu sahihi wa kuitoa ilipo na kuisogeza mbele na kwamba Pindi Chana yuko na timu ya watendaji mahiri na wachapakazi.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alimkaribisha Waziri Chana na kumpongeza kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo.

"Tunakukaribisha sana katika Wizara ya Maliasili na Utalii na kukupongeza sana kwa kuteuliwa kushika wadhifa wa Waziri wa Maliasili na Utalii," alisema Masanja.



Mkurugenzi wa Programu ya UCMAS Tanzania, Milli Rughani (kushoto), akimkabidhi tuzo Mary Gerald mwanafunzi wa Shule ya Msingi Montfort baada ya kushinda kipengele cha mshindi wa mahesabu ya kutumia vifaa katika mashindano ya kwanza ya kitaifa yaliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Kulia Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa Programu ya UCMAS, Roger Ohemeng, akiwa na mshindi wa mahesabu pasipo kutumia kikokotozi, Tutindaga Gwamaka ambaye ni mwanafunzi wa darasa la sita wa shule hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zitto Kabwe naye akabidhi kiti kwa Kinana

**Na Mwandishi Wetu**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amemaliza muda wake wa uongozi kwa nafasi ya Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) na sasa kinachukuliwa na Makamu Mwenyekiti mpya wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kanali mstaafu Abdulrahman Kinana.

Mkongwe huyo wa siasa za Tanzania anachukua nafasi hiyo ikiwa ni siku chache baada ya Mkutano Mkuu Maalum wa CCM kumchagua kwa kura zote kushika wadhifa wake huo mpya ndani ya chama hicho tawala Aprili Mosi, mwaka huu jijini Dodoma.

Uchaguzi huo ulifanyika kutokana na kujiuzulu kwa Phillip Mangula, huku chama hicho kikitumia nafasi hiyo kutangaza kuwasamehe baadhi ya makada waliokuwa wamefutiwa uanachama.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi wa TCD, Bernadetha Kafuko, Zitto atakabidhi rasmi kiti kwa Kinana keshokutwa.

Alisema TCD inawajulisha wanachama wake wote, wanachama washiriki (Associate Members), wadau wanaofanikisha kukamilika kwa Mkutano wa Haki, Amani na Maridhiano na wadau wengine wote wa demokrasia nchini kwamba maandalizi ya mkutano yanaendelea vizuri na kuwa mkutano unatarajiwa kufanyika tarehe 5 na 6 Aprili, mwaka huu kama kilivyoeleza awali katika taarifa zake.

Alisema kituo kinawahakikishia wadau wote na wananchi kwa ujumla kwamba ushirikiano ambao umekuwa ukitolewa na wadau wanaowezesha kufanyika kwa mkutano huo umekuwa wa kutia moyo na ni imani yao kwamba washiriki wote ambao wamekwishapewa taarifa ya kuhudhuria mkutano ambao utafanyika jijini Dodoma, hivi sasa watakuwa katika hatua za mwisho za maandalizi ya kuhudhuria mkutano huo muhimu ambao utatoa dira ya uimarikaji wa demokrasia nchini.

"Kituo kinatoa wito kwa wadau na vyama vya siasa kuendelea kuunga mkono juhudi za kuhakikisha kila mdau anasaidia kukamilika kwa mkutano huo ambao mafanikio yake yataleta tija siyo tu kwa wanachama wa kituo bali pia serikali na nchi kwa ujumla wake. "Jambo ambalo tungependa kuwahakikishia ni kwamba tumepata imani kubwa kuona namna gani wadau mbalimbali na hasa mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao nchini, wamekuwa na hamu kubwa ya kushiriki mkutano huu pamoja na ushawishi wao kwa taasisi mbalimbali za kimataifa katika kuunga mkono juhudi za kituo ili kufanikisha gharama za mkutano.

"Maandalizi yake yapo katika hatua za mwisho ambapo Kamati ya Ufundi ya TCD imekuwa bega kwa bega na watendaji wa kituo katika kukamilisha maandalizi yanayoendelea hivi sasa hapa Dodoma," alisema.

Alisema mkutano huu pia utashuhudia makabidhiano ya uongozi kutoka Chama cha ACT-Wazalendo kama Mwenyekiti wa sasa kwenda kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kama mwenyekiti mpya wa kituo.

"Hivyo, Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, atamaliza muda wake wa uongozi na kumkabidhi mwenyekiti mpya ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa CCM, Kanali mstaafu Abdulrahman Kinana, mnamo Aprili 6, mwaka 2022."

# Ashauri jukwaa la wadau wa mbegu

**Na Ibrahim Yassin,** NKASI

OFISA Kilimo wa Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, Okrani Chengula, amesema kutokana na umuhimu wa mbegu katika kilimo iko haja ya kuundwa kwa jukwaa la wadau wa mbegu.

Jukwaa hilo litakuwa na kazi kubwa ya kuhamasisha wakulima kupanda mbegu badala ya nafaka.

Amesema kwa sasa wakulima wengi wanalima kilimo cha mazoea kwa kutumia zana duni za kizamani zinazosababisha kupata mazao kidogo.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wadau wa kilimo wilayani humo na kueleza kuwa uzalishaji wa mazao mengi na wenye tija unategemea pia matumizi ya mbegu bora na sahihi ikiwamo kufuata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa maofisa kilimo.

Alisema jukwaa hilo licha ya kuhamasisha jamii kupanda mbegu sahihi lakini litakuwa na jukumu la kushawishi wadau kuweza kuzalisha mbegu mkoani Rukwa badala ya kutegemea mbegu zinazozalishwa nje ya nchi.

Mchambuzi wa Sera kutoka SAGCOT, Prudence Lugendo, alisema jukwaa la wadau wa mbegu endapo litatumika vizuri linaweza kutengeneza ajenda na kuwa karibu na watafiti na kuweza kuzalisha mbegu wenyewe.

Lugendo alisema jukwaa hilo litawashirikisha wadau mbalimbali zikiwamo taasisi za kifedha ambazo zinaweza kutoa mikopo kwa watu ambao watahitaji kuzalisha mbegu na kuacha kutegemea mbegu zinazozalishwa nje ya nchi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Nkasi, Pankrasi Maliyatabu, alisema endapo matumizi ya mbegu yatakuwa ni makubwa kuna uwezekano mkubwa kwa wakulima kuweza kuzalisha mazao na kufanya mapinduzi makubwa katika sekta hiyo ya kilimo

Hivyo, alilitaka jukwaa la mbegu lililoundwa kufanya kazi inayostahili ili jamii ijue umuhimu wa matumizi ya mbegu na kuachana na kupanda nafaka.

Mkutano huo ulifanikiwa kuunda jukwaa hilo la mbegu na kupata viongozi watakaloliongoza, kwamba Richard Maganga alichaguliwa kuwa mwenyekiti, huku Makamu Mwenyekiti akiwani Ladslaus Mzelela, Katibu akiwa Pirmin Matumizi, Katibu Msaidizi, Musa Ng'wani na Mtunza Hazina, Elia Siyame.

000000

## HABARI KITAIFA




Meneja Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael, akizungumza jijini Dar es Salaam jana, katika uzinduzi wa simu mpya aina ya Tecno Spark 8 kwa kushirikiana na kampuni ya Tecno. Kulia ni Mwakikishi wa TECNO, Joyce Kaswalala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TANROADS yawataka wakazi kutoiba alama za barabarani

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MENEJA wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Geita, Japherson Michael, amewataka baadhi ya wananchi wa mkoa huo kuacha tabia ya kuiba alama za barabarani.

Amesema kwa yeyote atakayebainika atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Alitoa onyo hilo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake na kueleza kwamba alama za barabarani ni muhimu, hivyo kila mwananchi awe mlinzi wa mwenzake kuhakikisha zinakuwapo ili kupunguza ajali.

Alisema endapo mwananchi akimwona mtu yeyote akikata au kuiba alama za barabarani atoe taarifa ofisi ya TANROADS Mkoa wa Geita au kituo cha polisi au ofisi ya mtendaji wa kata ili kukomesha vitendo hivyo vya uhalifu kwenye miundombinu ya barabara. Aidha, aliwataka wananchi wa Mkoa wa Geita kuchukua tahadhari kwa sababu barabara zinajengwa kwa kuzingatia viwango.

Michael alisema waendeshaji wa vyombo vya moto wakiona kuna sehemu hatarishi bado wana wajibu wa kuhakikisha kwamba wanachukua tahadhari ili kutokusababisha ajali kwa watu wengine.

Alisema sehemu za mjini hasa ndizo zimewekwa alama katika maeneo kwa ajili ya kuvuka barabara, kuwataka wananchi kuzitumia alama hizo kwa kadri inavyowezekana na kuchukua tahadhari zinazotakiwa.

"Kwa sababu wakati mwingine taa zimewekwa lakini hazifanyi kazi vizuri hivyo wananchi wanapaswa kuchukua tahadhari pindi wanapotaka kuvuka barabara," alisema. Alisema Barabara ya Mwatulole hadi Mtunduni yenye kilomita 2.4 imejengwa kwa lami na imekamilika, kwamba wataikabidhi kwa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) ili waweze kuweka matuta kupunguza ajali.

Pia aliwataka wananchi wa mkoa huo kuhakikisha sehemu za mizani inayohamishika wanachukua tahadhari wakati wa kuvuka barabara, kwa sababu mizani hiyo imewekwa ili kukomesha magari yanayokwepa kupima mizani.

# Pasaka kitaifa TEC kusaliwa mkoani Morogoro

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MHASHAM baba Askofu wa Jimbo Katoliki Morogoro, Lazarius Msimbe, amesema maadhimisho ya sikukuu ya Pasaka kwa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) yatafanyika kitaifa katika Kanisa la Mtakatifu Patris, mkoani humo.

Askofu Msimbe aliyasema hayo jana kwenye taarifa yake iliyosomwa kwa niaba yake na Padre Francis Korongo katika Misa ya Dominika ya nne ya Kwaresma iliyofanyika kwenye kigango cha Utatu Mtakatifu Parokia ya Mtakatifu Monica-Kihonda mjini hapa.

Askofu Msimbe alisema maadhimisho hayo yatafanyika katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Patris Morogoro yakianziwa na ibada ya Ijumaa Kuu kanisani hapo.

Akizungumzia Kwaresma Askofu Msimbe, alisema wakati huu wakristo hawana budi kuirarua mioyo yao ili kujenga jamii yenye usawa na iliyojaa upendo, undugu na umoja.

Alisema kila mmoja ana wajibu wa kutafakari nyenzo tatu alizowaachia mama Bikira Maria ambazo ni matendo ya Sala, kufunga na matendo ya huruma na kujiwekea mkakati mpya wa kuanza maisha mapya yampendezayo Mungu na watu.

Aidha, aliwataka viongozi wa makanisa kushirikiana katika maandalizi ya maadhimisho hayo ya Pasaka kitaifa yatakayofanyika Aprili 17, mwaka huu.

# Waiomba serikali kujenga vituo kulea watoto yatima

**Na Happy Severine,** BUSEGA

WATOTO yatima kutoka Kituo cha Bethany kilichoko wilayani Busega mkoani Simiyu, wameiomba serikali kuwekeza zaidi katika elimu na kujenga taasisi maalum za kulea na kusaidia watoto yatima kila mkoa.

Wamesema hatua hiyo itasaidia watoto wengi kupata msaada wa huduma za msingi kuliko hivi wanavyoendelea kuteseka mitaani na kuwa ombaomba.

Walitoa ushauri huo wakati wakipokea misaada kutoka katika Jumuiya ya Wanafunzi wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha Tawi la Simiyu.

Walisema watoto wengi wamekuwa wakikosa haki nyingi husani elimu bora kutokana na serikali kushindwa kuwapa kipaumbele kundi hilo.

Walisema endapo serikali itajikita na kupanua wigo zaidi wa elimu kwa makundi maalum wanaamini watoto yatima pamoja na wale wanaoishi katika mazingira magumu watapata haki sawa na watoto wengine.

Jacob Charles, alisema watoto wengi yatima waliotelekezwa wanashindwa kuziishi ndoto zao kwa kuwa siyo wote wanaopata msaada kutoka katika vituo vya kulea watoto.

Alisema wengi wanaangaika mitaani na kuangukia katika makundi mabaya ya wizi na uvutaji bangi pasipo wao kupenda.

Sarah Joseph mwanafunzi anayesomeshwa na kulelewa katika kituo hicho alisema wanatambua kuwa serikali haiwezi kushindwa kitu, hivyo waliomba serikali itambue jukumu la msingi la kuwasaidia watoto hao na kwamba wasiziachie taasisi binafsi kutekeleza majukumu hayo.

"Serikali haijawahi kushindwa kitu...tunaiomba ianzishe taasisi za serikali kwa kujenga vituo rasmi vya kusomesha na kuwalea watoto hao kwani hawana msaada mwingine zaidi ya kutegemea taasisi hizo binafsi...wanaamini serikali ikijenga vituo hivyo vya makuzi na malezi vitasaidia kupunguza tatizo hilo kwa kiasi kikubwa," alisema.

Mkurugenzi wa Kituo cha Bethany, Jesca Paul, alisema nguvu kubwa inahitajika katika kuwekeza kwenye vituo vya kulea watoto.

Alisema inatakiwa uwekezaji zaidi katika elimu kwa kila aina ya makundi ili kutoa fursa sawa kwa watoto wote.

Paul alisema mbali na jukumu walilonalo la kuwalea watoto hao ndani ya kituo chao bado wanakabiliwa na changamoto ya fedha, kwani mahitaji ya watoto hao ni mengi ukilinganisha na misaada wanayoipata kutoka kwa wafadhili.

## Shule ya Jokate yapaza sauti kikwazo cha maji

**Na Julieth Mkireri, KISARAWE**

SHULE ya Sekondari ya Wasichana ya Jokate Mwegelo iliyoko Kata ya Kibuta Wilaya ya Kisarawe inakabiliwa na kikwazo cha maji, hali inayosababisha wanafunzi kutumia muda mwingi wa kujisomea wenyewe kupata huduma hiyo.

Aidha shule hiyo ina uhitaji wa uzio kutokana na mazingira iliyoko ili kuweka ulinzi kwa watoto wa kike wanaosoma katika shule hiyo.

Kutokana na hali hiyo, uongozi wa shule pamoja na wanafunzi wameiomba serikali kuangalia na kutafuta namna ya kutatua kero hizo ili kuwalinda wanafunzi na madhara yanayoweza kujitokeza.

Wakizungumzia vikwazo vya shule hiyo juzi mkuu wa shule pamoja na wanafunzi walisema shule ina mazingira rafiki ya kujisomea, lakini kutokana na suala la uzio na vyanzo vichache vya maji serikali inatakiwa kuingilia kati kuvitatua.

Mkuu wa shule hiyo, Mariam Mpunga, alisema sekondari ya Jokate Mwegelo pamoja na kuwa na mazingira mazuri ya kujisomea kwa wanafunzi wa kike suala la uzio na kuongeza vyanzo vya maji ni vitu vya muhimu.

Mariam aliahidi shule hiyo kuwa na ufaulu wa juu katika mitihani yake ya kitaifa kutokana na eneo ilipojengwa na wanafunzi wake kujikita zaidi kwenye masomo wanayofundishwa.

Irene Sebastian na Husna Hamad, miongoni mwa wanafunzi wa shule hiyyo, walisema pamoja na kuwa na uhitaji mkubwa wa maji lakini suala la uzio ni la muhimu kwani shule imezungukwa na vichaka.

Naye Ofisa Elimu (vifaa na takwimu) wa Wilaya hiyo, Hassan Mathias, alisema shule hiyo ni mpya na bado kuna maeneo yanaendelea kufanyiwa marekebisho na kwamba upo mradi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) utapita katika eneo la shule hiyo na kumaliza kero iliyoko. Kwa mujibu wa ofisa elimu huyo, serikali inatambua vikwazo hivyo na iko kwenye mikakati ya kushughukiwa, na kwamba Mkurugenzi wa Halmashauri ameahidi kupeleka matangi kwa ajili ya kuvunia maji wakati utaratibu wa maji ya DAWASA ukiendelea.

Shule ya Sekondari Jokate Mwegelo ilianzishwa mwaka 2020 kufuatia ndoto ya viongozi ya kuhakikisha wanafunzi wa kike wanaondokana na kikwazo cha kukatisha malengo yao kielimu, kutokana na umbali wa shule ambao umekuwa ukisababisha baadhi yao kupata ujauzito.

# Serikali yatoa mbinu za kukabili ushindani ajira

**Na Christina Mwakangale**

SERIKÀLI imesema kwamba pamoja na cheti cha kitaaluma kuwa utambulisho wa mhitimu wa ngazi yoyote ya elimu ya chuo, programu za ujuzi na stadi za kazi, inahitajika kutokana na mahitaji na ushindani ulioko kwenye soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Imesema ni wakati wa taasisi kupitia mitaala ya mafunzo ya elimu, kuhakikisha inajumuisha ujifunzaji kwa vitendo, ikilinganishwa na sasa nadharia hutawala zaidi darasani.

Mkurugenzi wa Ukuzaji Tija kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Yohana Madadi, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye mahafali ya kozi fupi ya uanagenzi na kutunuku vyeti 105 kwa wahitimu wa Chuo cha Utalii cha Taifa (NCT), Kampasi ya Bustani, mkoani Dar es Salaam.

Alisema soko la ajira linamhitaji mtu mwenye ujuzi aliyejifunza kinadharia zaidi, na kwamba serikali ilibaini njia pekee ya kuwakuzia vijana ujuzi ni kupitia vyuo wanakojifunzia programu kwa njia ya uanagenzi inayotolewa na ofisi hiyo kwenye vyuo 72, nchini.

"Utafiti uliofanywa na serikali mwaka 2014, ulibaini asilimia 79.9 ya nguvu kazi ya taifa kiwango cha ujuzi kipo chini, asilimia 16.6 wa kiwango cha kati na asilimia 3.6 pekee ndio yenye ujuzi wa juu. Waajiri, wadau wengi husisitiza ujuzi ili kuwa na tija katika utoaji huduma.

"Uanagenzi ni programu inayohusisha vitendo kwa asilimia 60 na 40 ni nadharia darasani. Programu iko katika sekta ya usafiri na usafirishaji, TEHAMA, kilimo-biashara, ujenzi, nishati na madini, viwandani, utalii na ukarimu," alisema Madadi.

Kadhalika, alibainisha kupitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26), ofisi hiyo itatoa mafunzo ya kukuza ujuzi kwa vijana 581,000 kati yao 231,000 watajifunza programu ya uanagenzi.

"Katika awamu ya tatu ya programu ya taifa ya kukuza ujuzi ya uanagenzi, serikali imegharamia kulipia ada ya Sh. 450,000 kwa kila mhitimu, kwa wahitimu 14,440 kati ya hao 216 wanatoka NCT kampasi ya Arusha na Bustani," alisema.

Awali, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NCT, Dk. Shogo Mlozi, alisema chuo hicho kilianza kutekeleza programu hiyo tangu mwaka 2013 kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO) na sekta binafsi, na kwamba tangu kuanzishwa mafunzo hayo, wamepatikana wanagenzi 267 wakihitimu ngazi ya astashahada.

"Mafanikio ya programu hii tumebaini wahitimu wanapata ajira hata kabla ya kumaliza masomo, wanaiva ipasavyo. Baadhi yao wameajiriwa kwenye hoteli za hadhi ya nyota nne, tano zilizoko nchini," alisema Dk. Shogo.

Aliongeza kwamba, chuo hicho kutokana na uzoefu wa utoaji mafunzo ya uanagenzi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, iliwezesha udahili wa vijana 216 na kupata mafunzo hayo katika fani ya ukarimu ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri na kuajiriwa.

Kadhalika, Dk. Shogo alisema mafunzo ya vijana hao yalianza Julai mwaka jana, ambayo yalihusisha vitendo kwa asilimia 60, hususan kwenye mapishi, mapokezi, udobi, uokoji na kutoa huduma ya chakula na vinywaji.



Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Kimataifa la Afya la Fhi360, Waziri Nyoni (watatu kulia), akizungumza jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, wakati Benki ya Absa Tanzania ikikabidhi hundi yenye thamani ya Sh. milioni 10 kusaidia kampeni ya kuhamasisha Watanzania kupata chanjo ya COVID-19. Kutoka kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Mauzo ya Masoko ya Kigeni wa Absa, Irene Rwegalulira, Mkurugenzi wa Fedha Fhi360, Anselm Mmassy, Mkurugenzi wa Kampuni Kubwa na Uwekezaji wa Benki ya Absa Tanzania, Hugo Chilufya, Meneja Uhusiano ya Jamii wa Absa, Hellen Siria na Mshauri Mwandamizi wa Fhi360, Theresia Mrema. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shule binafsi Dar es Salaam zachuana Hisabati

**Na Gwamaka Alipipi**

WANAFUNZI zaidi ya 350 kutoka shule binafsi za Dar es Salaam wameshiriki katika shindano la kufanya mtihani wa Hisabati, ili kumpata mshindi wa somo hilo kupitia programu ya kuongeza usikivu, ubunifu, kumbukumbu na kujiamini (UCMAS).

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi baada ya kufungua shindano hilo, Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora wa Shule kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Euphrasia Buchuma alisema programu ya UCMAS ni nzuri na inafaa kuendelezwa pia katika shule za serikali.

Alisema katika Mkoa wa Dar es Salaam programu hiyo imezifikia shule chache za binafsi, hivyo alitoa wito kwa wahusika kuhakikisha programu hiyo inasambaa katika shule zote ili kumjenga mwanafunzi kiakili na kiuwezo.

"Hii programu ni nzuri kwa sababu inawalenga wanafunzi wenye umri kuanzia miaka mitano hadi 13, programu hii inamwezesha mwanafunzi kuwa makini wakati wote akiwa darasani. Pia inamjenga kiakili na kiuwezo kwa kufikiri kwa haraka," alisema Buchuma.

Alisema programu ya UCMAS inatoa elimu iliyokamilika ili kukuza umakini wa mtoto, fikra bunifu, uwezo wa kumbukumbu, kufikiri kimantiki na kuongeza kujiamini katika kukabiliana na changamoto.

"Ni jukumu letu sisi wazazi kutoa mazingira rahisi kwa watoto wetu ili kukuza uwezo wao. UCMAS inatoa mafunzo kwa wanafunzi wengi na inakuza na kupanua uwezo wao wa ubongo," alisema Buchuma.

Mkurugenzi wa UCMAS Tanzania, Milli Rughani, alisema programu hiyo imeanzishwa nchini Mei, 2018, kwamba mwaka huu ni mara ya kwanza kufanyika kwa shindano la mtihani wa hisabati kwa wanafunzi zaidi ya 350.

Alisema wanafunzi hao wametoka shule mbalimbali za binafsi katika Mkoa wa Dar es Salaam ili kuthibitisha uwezo wao wa kiakili kwa kujibu maswali 150 katika muda wa dakika nane.

Mwenyekiti wa Wawekezaji wa Elimu Tanzania, Mohammed Mringo, alisema: "Endapo serikali ikaipokea programu hii na kuiingiza katika silabasi ya elimu itasaidia sana kuwajenga wanafunzi kifikra na kuongeza uwezo wao kuwa kufikiria. Programu hii inamjenga mwanafunzi kuwa bora katika somo la hisabati ambalo limekuwa changamoto kubwa kwa wanafunzi wengi".

Mringo alisema wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wengi wanashindwa kufanya vizuri katika somo la Hisabati, hivyo kupitia programu hii itawawezesha wanafunzi kuwa na upeo mpana kwa kufikiria na kufanya vizuri katika somo hilo.

## SDF yanufaisha maelfu ya vijana

**Na Joseph Mwendapole**

VIJANA 31,984 wamenufaika na mafunzo ya kuendeleza ujuzi yanayotolewa na Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) tangu uanzishwe 2017.

Mfuko wa SDF uko chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na unaotekelezwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).

Mkugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuzye, alibainisha takwimu hizo wakati akifungua semina kwa waandishi wa habari kuhusu shughuli za mamlaka hiyo.

Alisema mfuko huo unaolenga kuwaendeleza vijana waweze kujiajiri baada ya kuhitimu masomo yao unatarajia kuwanufaisha vijana 38,000 mpaka kufikia mwezi Juni mwaka huu.

Alisema katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mpango wa mafunzo yaliyojikita katika sekta ya Kilimo na Kilimo Biashara, Sh. bilioni 3.1 zilitengwa kwa ajili ya kunufaisha taasisi 15 ambapo Sh. bilioni 2.9 zimetumika.

Alisema awamu ya pili ya utekelezaji wa SDF ilianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2019/20 na 2020/21, Sh. bilioni 9.7 zilitengwa kwa taasisi 81 za mafunzo kuwezesha wanufaika kupata ujuzi katika sekta sita za kipaumbele ambazo ni Kilimo na Kilimo Uchumi, Utalii na Huduma za Ukarimu, Uchukuzi, Ujenzi, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na Nishati.

"Hadi kufikia Machi 2022, TEA imetoa Sh. bilioni 8.1 kwa miradi 81 ambapo wanufaika 30,590 ikiwa ni wanaume 15,634 na wanawake 14,956 wamepatiwa mafunzo katika utekelezaji wa awamu ya pili," alisema.

Aidha, kupitia SDF, Sh. 385,779,984.20 zinatarajiwa kunufaisha vijana 1,018 katika mpango wa Uanagenzi na Utarajari katika sekta za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Utalii na huduma za ukarimu, Nishati, Ujenzi na Uchukuzi.

"Mfuko wa SDF pia unafadhili mafunzo kwa wanufaika 4,000 kutoka kaya maskini na makundi maalum hadi ifikapo Juni 2022. Hadi Agosti 2021, jumla ya wanufaika 1,627 walipata mafunzo katika awamu ya kwanza ya mpango huu," alisema.

Aliongeza kuwa awamu ya pili ya mpango wa ufadhili inatarajiwa kuanza mwezi Aprili 2022, ambapo wanufaika 2,373 wanatarajiwa kupata mafunzo kabla ya Juni 2022.

Alisema SDF pia uko katika hatua za mwisho kuanza kutekeleza ufadhili wa mafunzo ya kiubunifu kwa njia ya mtandao ambapo umelenga wanufaika 4,305 ifikapo Juni 2022.

Alisema Sh. bilioni 2.3 zitatumika kufadhili mradi huo na ruzuku ya shilingi 2,321,151,790.00 itawezesha utekelezaji wa mafunzo hayo.

# Wakala wa madeni kortini madai rushwa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

WAKALA wa Kampuni ya Adili Auction Mark ya kukusanya madeni ya Benki ya NMB, Brighton Macha (20) amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya Bukombe Mkoa wa Geita kwa makosa matatu ya kushawishi, kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 600,000 kutoka kwa Masanja Joseph.

Kosa hilo limedaiwa ni kinyume cha kifungu cha 301 na 302 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 Marejeo ya Mwaka 2019.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani mbele ya Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Ainawe Mushi, na aliposomewa mashtaka alikana, na yuko rumande kutokana na kukosa wadhamini.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili Kiongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Kelvin Murusuri, ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Mushi alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Aprili 12, mwaka huu kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali.

Aidha, aliyataja masharti ya dhamana ni kuwa na wadhamini wawili wenye barua ya utambulisho kutoka kwa ofisa mtendaji wa kata pamoja na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. 500,000 kwa kila mdhamini.

Hakimu Ainawe alisema mshtakiwa kwa kuwa hana wadhamini utaenda mahabusu hadi tarehe iliyopangwa, na kama utakuwa umewapata wadhamini basi utadhaminiwa kwa sababu dhamana yako ipo wazi.

Akisoma hati ya mashtaka Murusuri alidai kuwa kati ya Febuari na Machi mwaka huu, mshtakiwa alitenda makosa ya kushawishi hongo ya Sh. 600,000 kutoka Masanja ambaye ni mmiliki wa nyumba ambayo iliyokuwa inakusudia kuuzwa.

Alisema kosa la pili mshtakiwa huyo alipokea rushwa ya Sh 150,000 ikiwa ni sehemu ya fedha iliyokuwa imeombwa hapo awali Sh. 600,000 kutoka kwa Masanja ili achelewesha mnada wa nyumba hiyo ili arejeshe deni alilokuwa anadaiwa na Benki ya NMB iliyoko Bukombe.

Wakili huyo aliendelea kudai kuwa kosa la tatu mshtakiwa huyo alijipatia fedha kwa njia za udanganyifu kwamba ataahirisha mchakato wa kuuza nyumba hiyo kwa njia ya mnada.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Legal Services Facility (LSF), Lulu Ng'wanakilala (kulia), akikabidhi mfuko wenye hotuba fupi kuhusu masuala mbalimbali yaliyojadiliwa na wadau wa sekta ya msaada wa kisheria nchini kwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Pinda, wakati wa kufunga kongamano la Msaada wa Kisheria 2022 lililofanyika hivi karibuni jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri ataka ushirikiano watoa msaada kisheria

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Pinda, amewataka wadau wa msaada wa kisheria nchini kujenga na kuimarisha ushirikiano wa kimkakati na serikali, ikiwa ni fursa ya kuwasilisha mapendekezo mbalimbali yenye tija serikalini kwa lengo la kuboresha zaidi sekta ya msaada wa kisheria.

Kauli hiyo aliitoa mwishoni mwa wiki jijini Dodoma, wakati akifunga kongamano la siku mbili lililowakutanisha wadau wa sekta ya msaada wa kisheria takribani 120 kutoka Tanzania Bara na Visiwani.

Lengo la kongamano hilo ni kutathmini utekelezaji wa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017, pamoja na kuangalia huduma ya msaada wa kisheria kwa ujumla.

Pinda alisema serikali na wadau wa sekta ya msaada wa kisheria ni wadau muhimu katika utendaji kazi hasa katika sera, sheria, masuala mbalimbali ya haki ambayo yanawahusu wananchi.

"Ninaamini ili kuwapo matunda mazuri, kunahitajika uhusiano endelevu kati ya serikali na wadau wa sekta ya msaada wa kisheria. Kwa kutambua hilo nawahakikishia kuwa ofisi yangu itakuwa wazi kufanya kazi na wadau wa sekta ya msaada wa kisheria kwa kupokea taarifa, ushauri na mazungumzo mengine muhimu kuhusu mambo mbalimbali yanayowakabili wananchi katika sekta hii nyeti nchini," alisema.

Aliongeza kuwa serikali iko tayari kufanya kazi na wadau wa sekta ya msaada wa kisheria katika mazingira rafiki, huru, uwazi na usawa ili kusukuma mbele maendeleo ya sekta ya msaada wa kisheria kwakuwa lengo ni kujenga nchi moja.

Aidha, Pinda, aliwapongeza watoa huduma za msaada wa kisheria kwa kazi kubwa wanayoifanya katika jamii kwa kujitolea kwa lengo la kuwezesha jamii husani wale wasio na uwezo wa kupata huduma za msaada wa kisheria kupata usaidizi na utatuzi wa changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Legal Services Facility (LSF), Lulu Ng'wanakilala, ambao ndio waandaaji wa kongamano hilo kwa kushirikiana na wizara, alisema kuwa kongamano hilo la siku mbili lilijadili kwa kina masuala mbalimbali na kuibuka na maazimio ambayo baadaye kikosi kazi cha wadau kitaandaa ripoti na kuiwasilisha serikali kwa ajili ya utekelezaji zaidi.

"Kikao hiki kimetupa maazimio mengi. Niahidi kuwa wataalamu wetu wamerekodi yote yaliyojadiliwa na wadau. Baada ya kongamano hili timu hiyo itaandaa taarifa rasmi kwa ajili ya kuiwasilisha serikalini ili ifanyiwe kazi kwa ajili ya kuboresha na kuongeza ufanisi wa sekta ya msaada wa kisheria nchini," alisema Ng'wanakilala.

Vilevile, aliishukuru serikali kwa ushirikiano wao katika kuhakikisha inatoa mafunzo kwa watoa huduma za msaada wa kisheria na kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma hizi kwa wanawake na watoto, ambao ndio wahanga wakubwa na vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu.

Naye Mratibu wa Mtandao wa Watoa huduma za msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria nchini (TAPANET), Tolbert Mmassy, aliipongeza serikali kwa kuondoa ada ya usajili kwa watoa

Nipashe Spotika



XI WA THAMANI WALIOSHINDWA KUFUZU KOMBE LA DUNIA 2022 UK. 12-13



MAURICIO POCHETTINO

# KLABU 5 ZINAZOWEZA KUBADILISHA MAKOCHA

## ISIKUPITE

KIPA wa zamani wa England, David James, ndiye anayeshikilia rekodi ya kucheza penalti nyingi katika Ligi Kuu England. Kati ya penalti 63 alizokutana nazo, ameokoa 13, akifuatiwa na Thomas Sorensen ambaye ameokoa 12 kati 50 alizokutana nazo, wakati Mark Schwarzer akishika nafasi ya tatu kwa kuokoa penalti 10 kati ya 49 alizokutana nazo kwenye ligi hiyo pendwa duniani.



**LONDON,** England

MSIMU wa 2021-22 umetoa uzoefu tofauti kwa klabu bora katika Ligi Kuu tano kubwa za Ulaya. Licha ya matarajio, shamrashamra, uwekezaji na malengo kuelekea msimu mpya, baadhi ya mambo yaliishia kukatisha tamaa.

Bado imesalia miezi kadhaa kabla ya msimu kukamilika. Hata hivyo, baadhi ya klabu maarufu tayari zimeonyesha nia ya kutaka kuboreshwa zaidi.

Baadhi bado zinatatizika kupata ushiriki wao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, huku nyingine zikiwa hazina cha kupigania.

Tunapokaribia kipindi cha mwisho cha msimu, ni kawaida kwamba klabu zinafikiria kufanya maamuzi muhimu kabla ya msimu ujao. Wale ambao wamefurahishwa na kiwango bora wakati wa msimu watakuwa wakifikiria njia za kuimarisha zaidi timu zao.

Wale waliokatishwa tamaa, watakuwa na nia ya kufanya mabadiliko makubwa upande wao. Hiyo bila shaka itasababisha makocha kadhaa kupoteza kazi zao na wengine kuzichukua.

Hapa tunaziangalia klabu tano zinazoweza kufanya mabadiliko ya makocha wakati wa msimu wa majira ya joto yanayokuja, twende sasa...

### #5. AJAX

Kocha wa Ajax, Erik ten Hag hajawa na msimu mbaya. Hata hivyo, si mbaya kusema kwamba, Mholanzi huyo na timu yake wangefanya vema zaidi. Kwa sasa wanaongoza mbio za kuwania taji la Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, wakiwa na pointi 66, lakini ni uongozi finyu tu kwani PSV wanafuatia kwa karibu wakiwa na pointi 64.

Timu hiyo ya Uholanzi pia imetolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katika hatua ya 16-bora baada ya kufungwa na Benfica kwa jumla ya mabao 3-2. Kwa mujibu wa gazeti la The Metro, huu unaweza kuwa msimu wa mwisho kwa Ten Hag katika uwanja wa Johan Cruyff Arena.

Mtaalamu huyo analengwa zaidi na klabu kubwa nyingi Ulaya Ulaya, huku Manchester United ikishika kiti cha mbele. Inabakia kuonekana ni wapi atakuwapo msimu ujao.

### #4. JUVENTUS

Massimiliano Allegri aliteuliwa tena kuwa kocha wa Juventus msimu uliopita wa majira ya joto kwa lengo la kuirejesha klabu hiyo kwenye mstari ulionyoka. Walimaliza nafasi ya nne msimu uliopita, na kushindwa kutwaa taji la Serie A baada ya mfululizo wa miaka tisa.

Hata hivyo, kwa kuzingatia mafanikio ya timu tangu wakati huo, haitakuwa mbali kusema kocha huyo hajafanya lolote kufikia matarajio yaliyotarajiwa.

'Bianconeri' hao waliondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Villareal. Mbio zao kwenye Serie A pia hazijawa bora zaidi. 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin tayari kimetoka kwenye mbio za ubingwa na kwa sasa kinapigania kumaliza katika nafasi nne za juu katika msimamo. Mambo yakiendelea hivi, kuna uwezekano mkubwa kubadilishwa kocha mwishoni mwa msimu huu.

### #3. REAL MADRID

Miamba hii ya Hispania iliingia msimu huu ikiwa na kiwango bora kabisa kwenye LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya. Carlo Ancelotti alipata sifa nyingi baada ya timu yake kuilaza Paris Saint-Germain katika hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mapema mwezi uliopita.

Hata hivyo, 'Los Blancos' hao, walidhalilishwa kwa mabao 4-0 na Barcelona kwenye El Clasico mwezi uliopita katika Uwanja wa Santiago Bernabeu. Kwa hiyo, mazingira yanayomzunguka Ancelotti yamebadilika haraka. Kwa hali ilivyo, kuna hisia za kufadhaika taratibu zinakuja kwenye klabu hiyo.

Ancelotti atahitaji kufanya kila awezalo ili kuhakikisha Real Madrid wanachukua ubingwa msimu huu. Vinginevyo, kazi yake itakuwa chini ya tishio kubwa kabla ya msimu ujao.

### #2. MANCHESTER UNITED

Manchester United wanaonekana kuzidi kuingia kwenye mgogoro. Hata kurejea kwa Cristiano Ronaldo hakujatosha kuziba nyufa pale Old Trafford msimu huu. 'Mashetani Wekundu' hao wameshindwa kutamba uwanjani.

Kwa hali ilivyo, United itamaliza msimu wake wa tano bila ya kupata medali yoyote. Tayari wametoka katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England na pia wameondolewa katika mashindano yote ya mataji msimu huu.

Ralf Rangnick alichukuliwa kuwa kocha wa muda Novemba 2021 baada ya kufukuzwa kwa Ole Gunnar Solskjaer. Kwa mujibu wa mkataba wake, raia huyo wa Ujerumani anatazamiwa kuchukua nafasi ya ushauri hapo Old Trafford baada ya msimu huu. Hata hivyo, kwa mujibu wa gazeti la The Sun, klabu hiyo ilikuwa inafikiria kumpa nafasi ya kudumu ya ukocha msimu ujao.

Lakini nafasi yake ya kuteuliwa kama kocha wa kudumu mwishoni mwa msimu huu ni ndogo sana baada ya matokeo yasiyoridhisha. Kuna uwezekano mkubwa atatoa nafasi kwa kocha mwingine kuchukua utawala kipindi cha majira ya joto.

### #1. PARIS SAINT-GERMAIN

Kuiona PSG wakiwa kileleni mwa jedwali la Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, inaonekana si kitu ila ni udanganyifu tu. Ukweli ni kwamba 'Waparis' hao wanastahimili mambo magumu chini ya kocha Mauricio Pochettino. Kwa kweli, haitakuwa rahisi kusema huu ni moja ya misimu yao ya kukatisha tamaa kuwahi kutokea kulingana na mashabiki na wadadisi.

Paris Saint-Germain italazimika kulipa takriban Euro milioni 20 kama fidia ikiwa wataachana na Pochettino na wafanyakazi wake kufutwa kazi.

Miamba hao wa Ufaransa walitarajiwa kutoa tamko barani Ulaya baada ya dirisha la usajili la majira ya joto walilokuwa nalo. Walisajili wachezaji kama Lionel Messi, Gianluigi Donnarumma, Achraf Hakimi na Sergio Ramos msimu uliopita wa majira ya joto. Lakini waliishia kudhalilishwa tena na Real Madrid katika hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Pia walitupwa nje kwenye Kombe la Ufaransa baada ya kushindwa na Nice Februari mwaka huu. PSG wanajulikana kwa kuwa na subira ndogo sana linapokuja suala la kuwaondoa makocha. Kila kitu kinaonyesha kutakuwa na mabadiliko ya kocha pale Parc des Princes katika msimu wa majira ya joto.

# XI WA THAMANI WALIOSHINDWA KUFUZU KOMBE LA DUNIA 2022

**DOHA,** Qatar

KOMBE la Dunia la FIFA la 2022, halitakuwa na majina makubwa baada ya kuondolewa kwa nyota wengi katika kipindi cha miezi sita iliyopita.

Kipigo cha dakika za mwisho cha Italia dhidi ya Macedonia Kaskazini katika mechi ya mchujo wa kufuzu kilikuwa mshtuko mkubwa, hasa baada ya 'Azzurri' hao kutoka kutwaa ubingwa wa Ulaya (Euro 2020) msimu uliopita.

**Hata hivyo, nyota kutoka mataifa mbalimbali pia hawatashiriki kwenye Kombe la Dunia baadaye mwaka huu.**

Michuano hiyo ambayo imepangwa kufanyika nchini Qatar Novemba baadaye mwaka huu, haitakuwa na majina mengi makubwa. Nyota hawa wanaweza kuwa hawachezi nchi kubwa, lakini ujuzi wao binafsi unatosha kuonyesha kwamba wanapaswa kucheza katika mashindano makubwa zaidi duniani.

Katika makala haya, hebu tuangalie wachezaji 11 ambao wanathamani kubwa zaidi na hawatashiriki Kombe la Dunia 2022.

### GOLIKIPA: GIANLUIGI DONNARUMMA- EURO MIL. 65

Gianluigi Donnarumma alikuwa shujaa kwenye michuano ya Euro kwa Italia, lakini kwa bahati mbaya, mlinda mlango huyo hatashiriki Kombe la Dunia.

Kama ilivyotajwa hapo juu, Italia ililazimika kuifunga Macedonia Kaskazini kabla ya kucheza na Ureno au Uturuki katika mechi yao ya mwisho ya kufuzu. Lakini kwa mshangao wa kila mtu, walitolewa.

Donnarumma, ambaye amekuwa bora zaidi kwa mwaka jana, atalazimika kusubiri miaka minne zaidi kabla ya kuwa na matumaini ya kucheza katika mashindano makubwa zaidi ya mchezo huo. Kushindwa huku hakukuja wakati mzuri kwa kipa huyo, kwani PSG nao walitupwa nje kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### BEKI WA KATI: MILAN SKRINIAR - EURO MIL. 65

Milan Skriniar amekuwa beki bora wa kati kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kwa miaka kadhaa iliyopita. Hata hivyo, nyota huyo wa Slovakia hatakuwapo kwenye Kombe la Dunia mwaka huu.

Skriniar amechaguliwa kuwa Mwanasoka Bora wa Mwaka wa Slovakia kwa mwaka wa tatu mfululizo. Slovakia walikuwa na kundi gumu kupita, huku Croatia na Urusi zikiwa sehemu yake. Timu hizo mbili zilichukua nafasi ya kwanza na ya pili kwenye kundi, na kuiacha Slovakia ikiwa na uwezekano wa kutofuzu kwa mara ya tatu mfululizo. Lakini hili litakuwa ni majuto makubwa kwa mchezaji kama Skriniar ambaye amekuwa bora katika soka la ndani kwa kipindi cha nusu muongo uliopita.

Huku beki huyo akifikisha miaka 27 mwezi uliopita, atakuwa na matumaini ya kucheza Kombe la Dunia mara moja kabla ya kustaafu.

### BEKI WA KUSHOTO: DAVID ALABA- EURO MIL. 55

David Alaba amekuwa na kiwango bora kwa nchi na pia katika soka la klabu kwa muongo uliopita.

Ingawa Austria haijachukua taji lolote kwa muda mrefu, wamekuwa kwenye mashindano kadhaa. Pia walifika kwenye mechi za kufuzu, lakini hawakuweza kuifunga Wales.

Alaba sasa atakuwa na matumaini na Real Madrid lakini ikizingatiwa kwamba bado ana umri wa miaka 28, anaweza kupata nafasi nyingine ya kucheza Kombe la Dunia la 2026.

### BEKI WA KULIA: DAVIDE CALABRIA- EURO MIL. 25

Davide Calabria si mchezaji maarufu zaidi katika soka la dunia, lakini amefanya vema msimu huu. Beki huyo wa pembeni amefunga mabao mawili na kutoa asisti tatu katika mechi 19 za Ligi Kuu Italia, akiwa na AC Milan.

Hii ilimfanya kuwa sehemu ya kikosi cha Italia kilichopoteza katika nusu fainali ya Ligi ya UEFA dhidi ya Hispania Oktoba mwaka jana. Hakuwa sehemu ya kikosi cha sasa kilichoshindwa na Macedonia Kaskazini. Calabri angeweza kuingia kwenye kikosi ikiwa wangefuzu Kombe la Dunia.

Calabria angepiga hatua kama angefaulu katika mashindano makubwa ya kimataifa. Bila kujali, sasa atalazimika kusubiri miaka kadhaa kufanya hivyo.

### KIUNGO MKABAJI: MARCO VERRATTI- EURO MIL. 55

Marco Verratti kwa sasa ni mmoja wa viungo bora wa kati katika soka la dunia. Uchezaji wake huko Paris Saint-Germain ni ushahidi wa sawa na jukumu lake katika timu ya Taifa ya Italia.

Lakini, kwa mazuri yake yote, Verratti hakuweza kufanya vya kutosha kwa nchi yake dhidi ya Macedonia Kaskazini. Italia ilishinda michuano ya Euro miezi minane iliyopita, huku nyota huyo wa PSG akiwa sehemu muhimu ya kikosi hicho. Verratti, ambaye atafikisha umri wa miaka 30 mwaka huu, huenda asiweze kucheza tena Kombe lingine la Dunia.

### KIUNGO WA KATI: FRANCK KESSIE- EURO MIL. 42

Franck Kessie amekuwa na mchango mkubwa kwa AC Milan kwa miaka michache iliyopita, lakini hajaweza kutamba kwenye jukwaa la kimataifa.



HAALAND

Ivory Coast imekuwa na hali ya kutotulia kwa muda wa miezi sita. Walipoteza nafasi yao kwenye Kombe la Dunia la 2022 baada ya kufungwa na Cameroon, Novemba mwaka jana. Hii ni baada ya kuondolewa kwenye hatua ya 16-bora katika michuano ya AFCON mwaka huu.

Kwa hiyo, ingawa Kessie ametengeneza wakati mzuri nchini Italia na atajiunga na Barcelona msimu wa majira ya joto, hakutakuwa na jipya kwake kimataifa mwaka huu.

### KIUNGO WA KATI: NICOLO BARELLA- EURO MIL. 70

Nicolo Barella amekuwa mzuri sana kwa Inter Milan msimu huu, kama inavyothibitishwa na mabao yake mawili na pasi za mabao 10 katika mechi 27 za Serie A.

Barella kwa mwaka wa tatu mfululizo alijumuishwa katika XI bora zaidi cha Serie A.

Lakini kama mchezaji mwingine yeyote wa Italia kwenye orodha hii, Barella pia, hatashiriki Kombe la Dunia mwaka huu. Alikuwa sehemu ya kikosi cha kwanza kilichopoteza dhidi ya Macedonia Kaskazini hivi majuzi katika mchujo.

Ilistaajabisha kuona nyota huyo wa Inter Milan akionyesha kiwango duni sana katika mchezo huo, hasa baada ya Euro nzuri. Barella sasa itabidi asubiri kwa muda mrefu kabla ya Italia kufuzu Kombe la Dunia lijalo.

### KIUNGO MSHAMBULIAJI: MARTIN ODEGAARD- EURO MIL. 42

Mmoja wa nyota wawili wa Norway kwenye orodha hii, Martin Odegaard hatakuwa sehemu ya Kombe la Dunia nchini Qatar.

Odegaard anaonekana kuwa mchezaji bora ajaye wa Arsenal na hatakuwapo kwenye Kombe la Dunia. Kiungo mshambuliaji, ambaye alitimkia Arsenal majira ya joto yaliyopita, amekuwa mzuri sana kwa 'Washikabunduki' hao. Alishindwa kutoa uchezaji uleule wa kusisimua kwa Norway walipouhitaji wakati wa mchujo.

### STRAIKA: ERLING HAALAND- EURO MIL. 150

Hadi sasa mchezaji wa thamani zaidi kwenye orodha hii, Erling Haaland hatakuwapo kwenye Kombe la Dunia Novemba mwaka huu.

Nyota huyo wa Borussia Dortmund, amekuwa akifunga mabao ya kufurahisha kwa zaidi ya miaka miwili sasa. Ana mabao 80 katika mechi 82 za klabu hiyo ya Ujerumani.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 21, pia ana mabao 13 ya kimataifa katika michezo 16 aliyoichezea Norway. Lakini kutokana na jeraha la Novemba mwaka jana, hakuweza kufanya lolote kwa nchi yake kufuzu Kombe la Dunia.


### STRAIKA: PATRIK SCHICK- EURO MIL. 40

Patrik Schick ni mmoja wa wachezaji walio katika kiwango bora zaidi kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, kwa sasa. Lakini nyota huyo wa Bayer Leverkusen hatakuwapo kwenye Kombe la Dunia.


Jamhuri ya Czech ilitakiwa kuishinda Sweden kabla ya kucheza na Poland katika mechi ya mwisho ya kufuzu. Hata hivyo, walishindwa kufanya hivyo.

## Nukuu

"Sote tunajua kwamba shuti la Granit lina nguvu sana. Mashuti yake hayatabiriki sana, ni ngumu kudaka na si rahisi kwa kipa," **Kipa wa Arsenal Bernd Leno akielezea ugumu wa kudaka mashuti ya mchezaji mwenza wa timu hiyo, Granit Xhaka.**




"Sijafanya maamuzi yoyote hadi sasa, hakuna kilichofanyika. Naweza kuamua kesho, naweza kuamua siku ya dirisha la usajili, nataka kumaliza msimu vizuri, msimu huu bado haujaisha, lakini hatupo kwenye nafasi yoyote ya kuweza kushinda taji lolote, nahitaji kushinda mataji, kucheza kwa ajili ya kitu fulani, lakini kwa mwaka huu na michache iliyopita hatujafanikiwa kushinda taji lolote, inakatisha tamaa," **Kiungo wa Manchester United, Paul Pogba.**



"Ningependa Leo [Messi] arudi, lakini najua ni vigumu sana. Ana mkataba, jinsi alivyoondoka. Ikiwa Xavi [Hernandez] alimwambia kwamba milango iko wazi, nifikirie kama rafiki yake na mchezaji mwenzake. Ningempa kitambaa cha unahodha. Siku zote ananivutia na kumkubali," **Kiungo wa Barcelona, Sergio Busquets.**





Wachezaji wa Mabingwa Watetezi wa Kombe la FA Simba, Clatous Chama, Hassan Dilunga na Gadiel Michael wakipongezana baada ya kufunga moja ya mabao kwenye mechi iliyopita dhidi ya Dar City, wakishinda mabao 6-0. **PICHA: MAKTABA**

# MTIFUANO MKALI ROBO FAINALI FA

**Na Adam Fungamwango**

WIKIENDI ijayo Ligi Kuu Tanzania Bara itasimama tena kupisha robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF), maarufu kama Kombe la FA, itakayopigwa kwenye viwanja mbalimbali nchini kusaka timu zitakazokwenda nusu fainali kwa ajili ya kumpata bingwa.

**Mshindi wa kombe hili ndiye anayeiwakilisha moja kwa moja nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF).**

Timu nane ambazo zitakuwa dimbani kwenye mechi hizo za mtoani, ni mabingwa watetezi mara mbili, Simba, Yanga, Coastal Union, Kagera Sugar, Azam, Geita Gold, Pamba na Polisi Tanzania.

Makala haya tunaziangalia kwa uchache mechi hizo, pamoja na timu zinazokutana, haya sasa...

**YANGA VS GEITA GOLD**

Jumapili ijayo, ikimaanisha Aprili 10, mwaka huu, wanafainali wa msimu uliopita, Yanga watakipiga na timu ngumu isiyotabirika ya Geita Gold kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa katika robo fainali ya kwanza ya mchuano hiyo.

Yanga iliingia hatua hiyo kwa kuichapa Biashara United mabao 2-1, huku Geita Gold ikiidungua Mbuni kwa bao 1-0.

Ni mechi inayozikutanisha timu ambazo zimekuwa bora sana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sasa, Yanga ikiwa na mwendelezo mzuri, inaongoza ligi kwa pointi 48, huku wageni wao wakiwa kwenye nafasi ya sita kwa pointi 24. Hata hivyo, mwenye mechi zote mbili za ligi mzunguko wa kwanza na wa pili, Yanga ilishinda kwa bao 1-0 kila mchezo.

Timu zote mbili zitakuwa na mastraika hatari kwa sasa, Fiston Mayele mwenye mabao 10 mpaka sasa, Geita Gold ikiwa na George Mpole aliyefikisha mabao tisa.

Msimu uliopita Yanga ilitolewa hatua ya fainali kwa kufungwa na mabingwa watetezi wa kombe hilo, Simba bao 1-0 Julai 25 kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika Kigoma.

**COASTAL UNION VS KAGERA SUGAR**

Coastal Union itakuwa kwenye uwanja wake wa nyumbani, Mkwakwani Tanga, ikijaribu kulipa kisasi cha kufungwa mabao 2-1 kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu. Bado hazijakutana mzunguko wa pili. Mechi hiyo itakayochezwa Aprili 11, itakuwa ni kipimo tosha cha kocha aliyerudishwa Juma Mgunda, kuchukua nafasi ya Melis Medo.

Hata hivyo, timu hiyo itakabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa Kagera Sugar ambayo kwa siku za karibuni imeonekana kuwa tishio chini ya kocha Francis Baraza.

Coastal Union ilitinga hatua ya robo fainali ya Kombe la FA kwa kuifunga Mtibwa Sugar mabao 2-0, huku Kagera Sugar ikiidungua Namungo bao 1-0.

**SIMBA VS PAMBA**

Mabingwa mara mbili mfululizo wa michuano hiyo, Simba Aprili 13, mwaka huu watashuka kwenye dimba la Benjamin Mkapa kucheza dhidi ya Pamba ambao ni Mabingwa wa Ligi ya Muungano wa Tanzania mwaka 1990.

Itakumbukwa msimu uliopita, Simba ililitwaa kombe hilo kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, mjini Kigoma ilipoichapa Yanga bao 1-0 Julai 25, iliwekwa wavuni na Thadeo Lwanga.

Inaonekana kama vile mabingwa hao wamepata mchekea kwenye hatua ya robo fainali, lakini siku zote mpira ni dakika 90.

Iliingia hatua hiyo kwa kishindo baada ya kuirarua Ruvu Shooting mabao 7-0, Februari 16, mwaka huu. Katika hali ya kushangaza na ambayo haikutarajiwa na wengi, Pamba, yenye maskani yake Mwanza, iliiduwaza Dodoma Jiji kwa kuifunga mabao 2-1, Uwanja wa Nyamagana Mwanza.

Ndiyo timu pekee kati ya nane zilizotinga hatua ya robo fainali ambayo haipo kwenye Ligi Kuu.

Inacheza Ligi Daraja la Pili, kwa sasa inasaka tiketi kutinga ligi ya Championship.

**AZAM VS POLISI TANZANIA**

Siku hiyo hiyo ya Aprili 13, Azam itakuwa kwenye Uwanja wake wa nyumbani, Azam Complex kucheza robo fainali ya Kombe la FA dhidi ya Polisi Tanzania.

Azam, mabingwa wa misimu mitatu iliyopita, imekuwa ikiishia njiani misimu miwili mfululizo na mara zote inapokutana na Simba.

Misimu miwili nyuma, Julai Mosi 2020, ilifungwa mabao 2-0 kwenye hatua ya robo fainali msimu wa 2019/20, na msimu uliofuata ilipate tena bahati mbaya ya kukutana na Simba, ikachapwa bao 1-0 Juni 27 kwenye Uwanja wa Majimaji Songea lililowekwa wavuni na Luis Miquissone ambaye kwa sasa ametimkia kwa Mabingwa wa Afrika, Al Ahly ya Misri.

Azam ilitinga hatua hii kwa kuibamiza Baga Friends mabao 6-0, Polisi Tanzania ikiisulubu Prisons mabao 2-0.

Hata hivyo, Azam itabidi iwe makini kwani imepoteza mechi zote mbili za Ligi Kuu ilizocheza dhidi ya Polisi Tanzania kwa mabao 2-1 mzunguko wa kwanza Uwanja wa Ushirika Moshi Oktoba 2, mwaka jana, na bao 1-0, Machi 5, Azam Complex.

**JE, WAJUA?**

KLABU ya Simba imekuwa ya kwanza Tanzania kucheza mechi saa nne usiku hapa nchini katika historia ya soka la nchi hii. Simba ilifanya hivyo jana usiku kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya US Gendarmerie iliyoanza saa 4:00 usiku katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.



# HABARI DODOMA

## Simbachawene asisitiza haki katika kuongoza jamii

Na Augusta Njoji, DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Sera na Uratibu, George Simbachawene, amesema suala la haki ni la msingi katika kuongoza jamii na bila haki huwezi kuwa na taifa zuri.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki kwa Waziri mpya wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, kwenye hafla ya makabidhiano ya ofisi jijini hapa.

Katika mabadiliko madogo yaliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni, Waziri Simbachawene amehamishiwa Ofisi ya Waziri Kuu, Sera, Bunge na Uratibu huku Dk. Ndumbaro akihamishiwa Wizara hiyo kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo kwa sasa itaongozwa na Dk. Pindi Chana.

"Vipo vyombo vinavyoshughulikia na haki ambapo vipo chini ya wizara, baadhi ya changamoto ambazo nimeziona kwanza ni namna ambavyo wadau wa utoaji haki wanavyocheza na haki za watu, ni jukumu lao kuhakikisha haki inapatikana,"alisema.

Alibainisha kwa sasa watoa haki wanaangalia taaluma zaidi kuliko haki yenyewe.

"Bado kuna kazi kubwa nilikuwa nimeanza naamini na wewe (Dk.Ndumbaro) utapaendeleza, la pili ni mchakato unaomaliza jambo la haki, suala la haki kama ni kesi ya madai kwa mfano mtu aliyeshinda mahakamani anapata uamuzi wa mahakama,"alisema.

Alisema mahakama ndio inayoamua na kutoa uamuzi kwa anayestahili lakini uamuzi wa majaji na mahakimu wengi upo mikononi mwa wadau wengine wa haki hivyo haki ya mtu anayestahili hapewi hata kama mahakama ilishampa ushindi.

"Katika misingi ya utawala wa sheria mchakato wa haki ni hadi yule mwenye haki anapokabidhiwa haki yake mkononi haiwezi kutangazwa tu ndio haki inapatikana."

"Imekuwa ni utaratibu wa kawaida Mheshimiwa Waziri haki imetangazwa na mahakama kuwa ni mshindi lakini huyo mtu kufikia haki yake yaani kukaza hukumu kwa lugha nyepesi ni jambo gumu."

Alisema kesi zingine zinafika hadi Mahakama ya Rufani lakini zinarudishwa mahakama ya mwanzo, jambo hilo hilo lilikuwa ni moja ya vipaumbele alivyohudumu katika wizara hiyo.

Alieleza kuwa yapo mengi ambayo ameandika kwenye nyaraka za makabidhiano ambayo yanahitaji kushughulikiwa ili kuleta haki katika sheria.

Kwa pande wake, Dk. Ndumbaro alisema wizara hiyo ni muhimu katika uongozi na utawala wa nchi na kwamba atahakikisha anaendeleza maono yaliyoanzishwa na Waziri Simbachawene ili kushughulikia kero alizozibaini.

"Kuanzia Jumatatu (leo) idara zijipange kuniingiza darasani ya majukumu ya idara nijue mafanikio, changamoto na ushauri ili kusonga mbele na yale magumu kama aliyosema waziri hapa napenda yawekwe kwenye changamoto pale ili tushauriane," alisema.

Aliwataka wataalamu kuwa tayari kutoa ushauri anapopotoka.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maaridhiano Taifa, Alhaji Sheikh Dk. Mussa Salum (kushoto), akimkabidhi bendera ya jumuiya hiyo, Makamu Mwenyekiti wa Mkoa wa Dodoma, Zabibu Mtoro, kwa ajili ya utambulisho wa ofisi baada ya kufanyika mkutano mkuu wa wenyeviti na makatibu wa mkoa na wilaya, uliofanyika Dodoma juzi. (Wapili kushoto) ni Katibu Mkuu Taifa wa Jumuiya, Askofu Dk. Esrail Maasa, Mwenyekiti wa Mkoa wa Dodoma, Askofu Dk. Evance Chande, Katibu Mkuu wa Kamati ya Maadili, Prof. Emmanuel Shija (kulia). **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Wasichana 12,000 kurudishwa shuleni

Na Augusta Njoji, DODOMA

TAASISI ya Elimu ya Watu Wazima imepanga kusajili wanafunzi wa kike 12,000 ndani ya miaka mitano ikiwa ni kutekeleza Mpango wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) kupitia programu ya kuwarudisha wanafunzi hao kwenye madarasa ya sekondari.

Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Dk. Michael Ng'umbi, akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, alisema katika mpango huo wamejipanga kusajili wanafunzi 3,000 kila mwaka ambapo kwa mwaka huu lengo hilo limevuka kwa kusajili wanafunzi 3,118.

Dk. Ng'umbi alisema serikali imekuwa na wazo la kuwarudisha watoto wote shuleni hivyo moja ya programu zinazotekelezwa na serikali ni SEQUIP ambayo inashughulika na wasichana kuwarudisha katika madarasa ya sekondari na jukumu hilo limetolewa kwa taasisi hiyo.

"Mradi umeshaanza na mwaka wa kwanza ulikuwa wa maandalizi na mwaka huu ndio tumedahili kwa mara ya kwanza na ili kufikia lengo la wasichana 12,000 ndani ya miaka mitano tunahitaji kudahili wanafunzi 3,000 kila mwaka na mwaka huu tumedahili wanafunzi 3,118 ambao ni zaidi ya lengo," alisema.

Alisema mafanikio hayo yametokana na ushiriki mkubwa wa maofisa elimu ya watu wazima na viongozi mbalimbali mpaka ngazi ya kata.

Hata hivyo, alisema serikali imekuja na mkakati wa kujenga madarasa ya kisomo cha elimu ya watu wazima nchi nzima ili kutoa stadi za kusoma na ujuzi.

"Tungependa madarasa ya kisomo kwa watu wazima yaanzishe kila mahali na ndio maana tumeamua kuwajengea uwezo maofisa elimu wa watu wazima ili programu hii iweze kuwa na ufanisi," alisema.

Alitoa wito kwa Watanzania kuchangamkia fursa elimu ya watu wazima na kisomo kwa watu wazima hasa kutokana na kuwa kisomo hicho hakijajikita kwenye kusoma, kuandika na kuhesabu bali kuibua fursa za kiuchumi kama kilimo na biashara.

## Utafiti waanza wa viashiria magonjwa yasiyoambukiza

Na Paul Mabeja, DODOMA

MGANGA Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, amesema serikali inafanya utafiti wa viashiria vya magonjwa yasiyoambukiza nchini na inatarajia kutoa taarifa yake mwishoni mwa mwaka huu.

Aidha, amesema katika kukabiliana na magonjwa hayo, serikali itahakikisha inaimarisha upatikanaji wa vifaa tiba, vitendanishi na dawa kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali za rufani za mikoa.

Dk. Sichalwe, alibainisha hayo jana alipokuwa akifunga mafunzo ya kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza kwa watoa huduma za afya kutoka mikoa nane ya Tanzania Bara. "Nyie wataalamu pia mnatakiwa kuendelea kufanya utafiti unaohusu magonjwa haya, mpate ushahidi utakaowasaidia wafanya uamuzi na kuchukua hatua katika kukabiliana na magonjwa haya," alisema.

Alisema ili kukabiliana na magonjwa yasiyo ambukiza nchini serikali itaimarisha upatikanaji wa huduma za vifaa tiba, vitendanishi pamoja na dawa ili wananchi wapate huduma katika maeneo yao.

"Tunakwenda kuimarisha upatikanaji wa vifaa tiba, vitendanishi pamoja na dawa kwa ajili ya magonjwa haya kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali za mikoa ili kama mtu anahitaji kupima sukari basi apime pia kama ataka kupima pressure apime palepale," alisema Dk. Sichalwe.

Vile vile, aliwataka wananchi kufanya mazoezi na kuepuka matumizi ya tumbaku, pombe kupita kiasi, chumvi nyingi ili kujilinda na magongwa hayo.

Kwa upande wake, Meneja Mpango wa Taifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa yasiyoambukiza, Valeria Millinga, alisema serikali imeandaa mpango mkakati wa tatu wa kitaifa wa kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza, mwaka 2021 hadi 2026. "Mkakati huu unatekelezwa kwa kuzingatia vipaumbele vya Mpango Mkakati wa Afya (Health Sector Stratergic Plan) ya mwaka 2021 - 2026 inayolenga kuimarisha mifumo ya utoaji huduma za afya".

"Lengo ni kuboresha kiwango cha huduma za kinga, tiba na huduma utengamao za magonjwa hayo kuanzia ngazi ya jamii mpaka taifa," alisema.

Kadhalika, alisema moja kati ya mikakati iliyoko ni kuvijengea uwezo vituo vya afya 600 kwa kuwapa mafunzo watoa huduma za afya juu ya utoaji wa huduma za kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyo ambukiza.

"Mafunzo haya yanategemea kuwafikia watoa huduma za afya msingi wapatao 3,000 kutoka mikoa 26 kufikia Desemba, 2023 kupitia Mpango wa Taifa wa Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza kwa kushirikiana na Tanzania Diabetic Association (TDA) na OR-TAMISEMI," alifafanua.

Aliongeza kuwa taasisi hizo ziliandaa mtaala wa utoaji wa mafunzo ya magonjwa yasiyoambukiza kwa watoa huduma ngazi ya afya msingi (vituo vya afya).



## Walimu walilia miundombinu rafiki shuleni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WALIMU mkoani Mbeya, wameiomba serikali kuwapangia vituo vya kazi ambavyo miundombinu yake imekamilika ili kuongeza ufanisi wa ufundishaji na kuongeza ufaulu wa wanafunzi.

Wanadai kuwa wakati mwingine ufanisi unakuwa mdogo kutokana na miundombinu.

Aidha, wameiomba serikali kuondoa kero za ucheleweshaji wa baadhi ya stahiki zao ikiwamo malipo ya likizo na uhamisho ili kuwaondolea manung'uniko ambayo yanaweza kupunguza ufanisi kwenye utendaji kazi.

Katibu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Mkoa wa Mbeya, Sekela Malaga aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha baraza la chama hicho kilicholenga kujadili matatizo mbalimbali yanayowakabili walimu.

Alisema walimu wengi hasa wanaopangiwa vituo vya kazi kwenye shule mpya huwa wanakabiliwa na wakati mgumu hasa wanapolazimika kufundishia wanafunzi kwenye vyumba vya madarasa ambavyo havijakamilika.

Alisema hali hiyo huwa inawafanya walimu kutokuwa na morali nzuri ya ufundishaji na hivyo kupungua kwa ufanisi wa ufundishaji hali inayopunguza hata ufaulu wa wanafunzi.

"Walimu tuna kazi ngumu sana, mwalimu anapangiwa shule mpya, lakini akifika huko anakuta mazingira magumu, miundombinu haijakamilika, nyumba za kuishi hakuna na vitu vingine muhimu, hii inakatisha tamaa mno," alisema Sekela.

Vilevile aliiomba serikali kuacha kuwalazimisha walimu kupokelea mishahara yao kwenye benki za kibiashara na badala yake watumie Benki ya Mwalimu Commercial Bank (MCB).

Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Mbeya, Nelusigwe Kajuni, alisema sekta ya elimu ni miongoni mwa sekta muhimu kwa ajili ya maendeleo ya taifa kutokana na kuzalisha wataalamu hivyo ni lazima iangaliwe vizuri hasa maslahi ya walimu.

Alisema walimu wanapokuwa na malalamiko mengi wanashindwa kufanya kazi vizuri kutokana na kutumia muda mwingi kuhangaika namna ya kutatua shida zao badala ya kufanya kazi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema serikali inatambua matatizo yanayowakabili walimu na inaendelea kuyashughulikia ili kuhakikisha kundi hilo linafanya kazi kwa uhuru na katika mazingira ambayo ni rafiki.

Alisema walimu ndio walioshikilia maendeleo ya walimu, hivyo wao ndio wanaweza kuwafaulisha ama kuwafelisha, hivyo akaahidi kuendelea kushirikiana nao kutatua baadhi ya kero ambazo zinatatulika katika ngazi ya mkoa na zinazohitaji viongozi wa kitaifa wataziwasilisha.

# Wachungaji KKKT Konde waanza kutimuliwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOGORO unaoendelea ndani ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Konde, umeuchukua sura mpya, baada ya baadhi ya shirika waumini kuanza kuwatimua wachungaji wanaomuunga mkono aliyekuwa Askofu wa Dayosisi hiyo, Dk. Edward Mwaikali.

Mwishoni mwa wiki waumini wa kanisa hilo Usharika wa Mbalizi, walimpa mchungaji wao, Atupele Malawa saa 12 awe ameondoka katika kanisa hilo wakidai kuwa yeye ni miongoni mwa waanzilishi wa mgogoro huo.

Waumini hao walichanga fedha na kukodi gari kwa ajili ya kumsafirisha mchungaji huyo na familia yake, lakini mwenyewe akalikataa kwa maelezo kuwa alikuwa ameambiwa na viongozi wa Dayosisi kwamba wao ndio wangempatia gari kama walikuwa na nia ya kumsafirisha.

Kiongozi wa waumini hao, Godfrey Mwasuku, alisema wanamtuhumu mchungaji huyo kuwa kinara wa mgogoro huo kwa sababu yeye ndiye alikuwa mwenyekiti wa kamati iliyokuwa inaratibu kuhamisha Makao Makuu ya Dayosisi kutoka Tukuyu wilayani Rungwe kwenda jijini Mbeya.

Alisema uhamisho huo wa dayosisi ndio kiini cha mgogoro huo, na kwamba mchungaji huyo amekuwa hatoi matamko ya kueleweka kuhusu mgogoro huo zaidi ya kuwataka waumini waiombee dayosisi ili itengamae.

"Anatutaka tuiombee dayosisi wakati yeye mwenyewe anajulikana yuko upande wa Dk. Mwaikali na ndiye alikuwa anaratibu kuhamisha kiti kutoka Tukuyu kuleta Mbeya Mjini. Sisi tumeona kazi ni ngumu na hivyo tumeona hatuwezi kuendelea kuwa naye," alisema Mwasuku.

Naye Peter Mwakisambwe alisema mbali na mchungaji huyo kuwa kinara wa mgogoro huo, pia amekuwa akihujumu miradi ya kanisa hasa mradi wa gari la kubeba abiria ambalo tangu walipolinunua hawajawahi kusomewa mapato na matumizi na alipeleka nyaraka za uongo serikalini.

Alisema Mchungaji huyo alipeleka nyaraka Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) zinazoonyesha kwamba kanisa hilo linamiliki pikipiki ya magurudumu matatu (bajaji) wakati wao wanamiliki gari hali ambayo walihisi alilenga kuiibia serikali na kanisa.

Alisema kutokana na matatizo hayo. waliamua kuitisha kikao pamoja naye ambacho walikubaliana aondoke ushirikani hapo ili akahudumu sehemu nyingine, na kwamba yeye mwenyewe aliridhia na kuwaomba wamwandalie gari. Alisema walimpatia saa 12 aondoke, lakini walipoleta gari la kubeba mizigo alilikataa na baadaye amechukuliwa na mchungaji wa Nzovwe wakaondoka na kufunga milango ya nyumba.

"Tumeleta gari la kwanza akalikataa, tumeleta la pili akaondoka na kufunga milango, sasa kama anang'ang'ania hapa atamhudumia nani wakati sisi kama waumini hatumtaki?" Alisema Mwakisambwe.

Naye Roda Mwakajinga alisema kutokana na mgogoro uliopo kati ya mchungaji huyo na waumini, idadi kubwa ya waumini wameacha kuhudhuria kanisani na kwamba hata mapato ya kanisa yameanza kushuka.

Alisema ili kunusuru hali hiyo, ndio maana waliamua kumtimua mchungaji huyo ili waanze upya kulitengeneza na kwamba wanaendelea na maombi ili mgogoro huo uishe na kanisa litengamae.

Hata hivyo Nipashe lilifika nyumbani kwa mchungaji huyo, Mlawa kwa lengo la kutaka kujua msimamo wake, lakini akakataa kuzungumza kwa maelezo kuwa hakuwa vizuri kuzungumza kutokana na kuvurugwa na mgogoro huo.



Baadhi ya wadau wa elimu wakiwa pamoja baada ya kumalizika kwa mdahalo wa wadau wa elimu jumuishi ulioandaliwa na Shirika la Iringa Development of Youth Disabled and Children Care (IDYDC) kupitia mradi wa Elimu Jumuishi kwa ufadhali wa Internews Tanzania jana. **PICHA: FRODAY SIMBAYA**

# Serikali yawakosha wakulima wa parachichi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa maparachichi katika Wilaya ya Rungwe, wameishukuru serikali kwa kuondoa baadhi ya tozo za zao zilizowafanya wanunuzi kuacha kununua matunda yao na kukimbilia maeneo mengine yenye masharti nafuu.

Miezi ya karibuni matunda ya wakulima yalikuwa yamekosa soko, hivyo kuanza kuharibika baada ya baadhi ya wanunuzi kukimbia vikwazo vilivyokuwapo hali ambayo ilikuwa inawasababishia wakulima hasara.

Wakizungumza na waandishi wa habari wakulima hao waliiomba serikali kuongeza juhudi ya kuwatafutia wanunuzi ili kuepusha hasara kuendelea kuwa kubwa katika kipindi hiki ambacho wanunuzi hawana taarifa za kuondolewa kwa tozo.

Mmoja wa wakulima hao, Solomon Mwakapenda, alisema wakulima walikuwa wanapata shida kutokana na serikali kuwapangia wanunuzi badala ya kuwaacha wawe huru na kilimo chao.

Alisema walikuwa wanalazimishwa kwenda kupokea malipo yao kwenye taasisi za kifedha hasa benki ama kwenye ofisi za baadhi ya kampuni, hali ambayo alidai ilikuwa inawakwaza kutokana na kuwa na milolongo.

"Mimi nimeongea na mnunuzi nikiwa nyumbani ama shambani, tunachuma matunda anapakia halafu naambiwa nikachukulie hela benki, sasa huwa tunaogopa kutekwa ama kudhurumiwa, kwa sasa tunaishukuru serikali imetupa uhuru," alisema Mwakisambwe.

Alisema katika kipindi ambacho wakulima walikuwa wamewakimbia, wameingia hasara kutokana na baadhi yao kulazimika kuwauzia walanguzi ambao walikuwa wananunua gunia moja kwa Sh. 30,000.

Naye Jafary Isyaka alisema katika kilimo cha zao hilo wanunuzi walikuwa wanatozwa Sh. 150 kila kilo ambazo Sh. 50 ilikuwa kwa ajili ya kuchumia, Sh. 50 kwa ajili ya kusafirisha na Sh. 50 kwa ajili ya Chama cha Ushirika.

Alisema kutokana na hali hiyo wanunuzi waliona kwamba ni gharama kubwa kununua matunda hayo wilayani Rungwe kuliko maeneo mengine nchini na hivyo wakaamua kukimbia na kuwaachia kilio wakulima.

Alisema wanunuzi wengi walikimbilia katika mikoa ya Njombe na Songwe ambako masharti ya ununuzi wa zao hilo ni nafuu na hivyo wao wakakosa soko kabisa.

Alisema wakulima wamekuwa wakitumia gharama kubwa kwenye uzalishaji wa zao hilo bila kusaidiwa na serikali, lakini wakati wa kuuza wanaanza kupangiwa masharti magumu.

"Tunamshukuru Mkuu wa Wilaya ametupa uhuru wa kuuza matunda yetu tunakotaka sisi, kama mnavyojua mbolea bei ziko juu lakini wakulima tunajikongoja tunanunua, tunanunua miche kwa bei na huduma zingine, lakini anajitokeza mtu anakuja kutuletea masharti wakati wa kuuza," alisema Isyaka.

Kwa upande wake Boniface Mwakabungu alisema maparachichi ni miongoni mwa mazao ambayo yanatakiwa yakishakomaa yachumwe haraka na kuuzwa kwa maelezo kuwa yanaharibika ndani ya muda mfupi yasipochumwa.





# Hamad aeleza kilichomrudisha CUF

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), Hamad Masoud Hamad, amesema kurudi kwake katika chama hicho ni kujenga chama imara, na kwamba chama hicho sasa kitakua tishio kwa vyama vyingine vya siasa.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari makao makuu ya chama hicho Mtendeni Mjini Zanzibar baada ya kurejea kutoka Dar es Salaam katika mkutano mkuu wa chama hicho na kupewa wadhifa huo.

Hamadi ambaye alichaguliwa hivi karibuni kushika wadhifa huo baada ya kujitoa ACT- Wazalendo, alisema kuwa kurudi kwake CUF ni kama samaki aina ya kambare aliyekuwa nje ya maji na ukimrudisha huogelea.

Alisema miongoni mwa vipaumbele vyake ni kurejesha hadhi ya chama hicho na kukiimarisha ili kuwa na wanachama wengi zaidi na kuchukua dola katika Uchaguzi Mkuu wa 2025.

"Chama hiki hakifi kwa namna kilivyoundwa labda kiumwe na kusinzia na kwa sasa mkakati wake ni kuondoa tofauti zilizopo ili kuelekea uchaguzi mkuu wa 2025 na kufanya vizuri," alisema Hamad.

Kiongozi huyo aliyekuwa CUF kwa muda wa miaka 27 kabla ya kuingia ACT- Wazalendo, alisema kukaa katika chama hicho kwa miaka mitatu amejifunza mambo mengi ikiwamo kuwafahamu viongozi wa asili wa chama hicho.

"Kitu ambacho nimejifunza na kukiona iwe kizuri au kibaya ni kuwajua viongozi wa ACT. Sitowaambia nimewajua vipi hao viongozi lakini nikuambieni kuwa yapo mazuri sana na yapo mabaya sana," alisema.

Alisema watu wengi waliondoka CUF na kwenda ACT -Wazalendo kutokana na mapenzi ya marehemu Maalim Seif ambaye alikuwa na ushawishi mkubwa wa kisiasa lakini sio kwa ridhaa yao.

Aliwakaribisha wanachama wanaotaka kujiunga na chama hicho wachukue fomu mapema ili uchaguzi wa chama ukianza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

"CUF kumenoga ruduni kwenu msiogope...wakati ndio huu uchaguzi wetu mkuu wa chama unaotarajiwa kufanyika mwezi ujao ni wa huru na haki," alisema Hamad.

# Wizara yafagilia mfuko huduma ya afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema kuwapo kwa mfuko wa huduma za afya kutasaidia kuleta ufanisi na kuwawezesha wananchi kupitia kupata matibabu bora.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Sera wa Wizara ya Afya, Dhamira Mohamed, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu nia ya serikali kuanzisha mfuko huo.

Alisema Serikali ya Zanzibar inatumia Sh. bilioni 20 kwa mwaka kwa ajili ya gharama kuendesha huduma za afya ikiwamo ununuzi wa dawa.

Alisema kiwango hicho cha fedha kinaweza kupunguwa kama serikali itafanikiwa kuanzisha huduma za afya na kuyafikia makundi yote ikiwamo watu binafsi.

"Tunahitaji huduma za afya za uhakika ambazo zitatolewa kwa wananchi wanaofika katika vituo vya afya kupata tiba za maradhi mbalimbali nchini," alisema.

Naye Ofisa Mwandamizi Wizara hiyo, Yassin Ameir, alisema mfuko wa huduma za afya ni muhimu ambao utakapoanzishwa utafanikiwa kuyafikia makundi mbalimbali ikiwamo sekta binafsi.

Kwa upande wake Ofisa Afya wa Wizara ya Afya, Abdilahi Haji, alisema kuanzishwa kwa mfuko wa huduma za Afya kwa kiasi kikubwa utasaidia kuimarisha huduma hizo hadi vijijini ikiwamo kupatikana kwa vipimo sahihi.

Alisema miongoni mwa changamoto kubwa inayoikabili sekta ya afya ni pamoja na ukosefu wa vipimo ambavyo vinahitajika kwa wananchi wanaofika katika hospitali kupata huduma za afya.

Alifahamisha ujenzi wa hospitali 10 za Wilaya ya Unguja na Pemba kwa kiasi kikubwa utazingatia vipimo vya magonjwa mbalimbali ambapo wananchi wanapofika katika hospitali hizo huduma hizo zipatikane.

"Changamoto kubwa inayoikabili sekta ya afya kwa sasa ni kukosa kuyafikia makundi mbalimbali muhimu katika kupata huduma za afya ambapo jibu la suala hilo ni mfuko wa huduma za afya," alisema.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipo katika mchakato wa kuanzishwa kwa huduma za bima ambao lengo lake kubwa kuyafikia makundi yote muhimu ya wananchi wa Zanzibar katika afya ya jamii.



Mkuu wa Idara ya Sheria Chuo cha Mafunzo Zanzibar, Yussuf Maabad Makungu (aliyesimama), akizungumza na wadau walioshiriki hafla ya uzinduzi wa Jumuiya ya Mapambano dhidi ya Vitendo vya Kihalifu Zanzibar (JMVUZ) iliyofanyika ukumbi wa Chuo cha Mafunzo (Magereza), Kilimani mjini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yaombwa vyeti kwa wafungwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imeshauriwa kuanzisha mchakato wa kutoa vyeti maalum kwa wafungwa wakiwa wanatumikia kifungo magerezani ili viwasaidie katika fursa za ajira. Ombi hilo lililotolewa na Mkuu wa Idara ya Sheria Chuo cha Mafunzo Zanzibar (Magereza), Yussuf Maabad Makungu, katika hafla ya uzinduzi wa Jumuiya ya Mapambano dhidi ya vitendo vya kihalifu Zanzibar (JMVUZ) iliyofanyika ukumbi wa Chuo cha Mafunzo Kilimani mjini Zanzibar.

Alisema wanafunzi wa vyuo vya mafunzo (wafungwa) wameandaliwa utaratibu maalum unaowawezesha kujifunza fani tofauti, hivyo ni vyema fani zao kutambulika kwa kupewa vyeti hasa kesi zao zinapomalizika na kurudi uraiani.

Maabad alisema ni jambo la kupongezwa kuwa na jumuiya iliyowakusanya pamoja watu walioingia katika mfumo wa kijinai na kuhukumiwa lakini wakaweza kuanzisha chombo cha kuwasemea na kupigania maslahi yao.

Kwa upande wake, Said Suleiman Ali, Mratibu wa Jumuiya ya Mapambano dhidi ya vitendo vya kihalifu Zanzibar (JMVUZ) alisema malengo ya jumuiya ni kuhakikisha vitendo vya kihalifu vinavyofanywa na watu wa makundi mbalimbali vinaondoka Zanzibar.

Alisema mapambano ya kuondoa uhalifu kupitia jumuiya yao yatajikita zaidi katika kurekebisha tabia za wanajamii kwa kueleza mambo mbalimbali yanayopelekea watu kupata hukumu ya kifungo gerezani.

Alifahamisha kuwa wanachama wa Jumuiya hiyo ni wale wote waliowahi kuhukumiwa vifungo au kukaa rumande kwa zaidi ya miezi sita.

"Kwa vile wanachama wetu wengi ni wale waliowahi kupata hukumu ya kifungo, bila shaka watakuwa na ushuhuda mwingi wa kuieleza jamii ili nao waepuke kufanya matendo ya kihalifu," alisema Mratibu Said.

Alisema wafungwa wanapokuwa katika vyuo vya mafunzo hukumbana na mengi ikiwamo kukosa huduma zao muhimu hivyo, Jumuiya itakuwa mstari wa mbele kutetea maslahi na haki zao wanapokuwa ndani au nje ya vyuo vya mafunzo.

Said alisema jambo jingine watakalolipa kipaumbele katika jumuiya hiyo ni kuhakikisha wanatoa msaada wa kuwapatia wanasheria na mawakili ili kuwatetea wanachama wao.

Alisema wanakusudia pia kupambana na dhana mbaya iliyojengeka katika jamii dhidi ya watu waliowahi kupitia vyuo vya mafunzo na kunyooshewa vidole pale wanapopita mitaani.

"Fikiria mtu anahukumiwa kifungo cha miaka 30, bila shaka kila jambo lake huharibika, akirudi mtaani anaanza maisha mapya yaliojaa ugeni. Sisi kama jumuiya lengo letu ni kukutana na watu hao kuwajenga vyema kimawazo ili wakitoka wasiwe wageni wala wasitengwe," alisema Mratib Said.

# GGML yapiga jeki afya ya uzazi CCBRT

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya AngloGold Ashati kupitia mgodi wake wa dhahabu Geita (GGML) imetoa Sh. milioni 50 kwa Hospitali ya CCBRT ili kusaidia na kuboresha huduma za afya ya uzazi.

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam katika hafla ya kukabidhi hundi kwa niaba ya AngloGold Ashanti, Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Kampuni ya GGML, Stephen Mhando, alisema msada huo ni moja ya majukumu ya kampuni hiyo kutekeleza mpango wake wa uwajibikaji kwa jamii.

Alisema GGML inaunga mkono mipango ya serikali na wadau wengine kuhakikisha kwamba watu wote wanaishi kwa amani na ustawi, jambo ambalo linawezekana ikiwa watu wengi wana afya njema.

Alisema mchango huu wa Sh. milioni 50 unakamilisha mojawapo ya maadili ya msingi ya kampuni yao katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na mustakabali endelevu kwa jamii.

"GGML inatekeleza kikamilifu miradi mbalimbali ya kijamii ambayo imesaidia pia kuboresha za afya. Kwa kuanzia, malengo yetu yalijikita katika kupunguza maradhi ya malaria nchini ambapo GGML imeungana na wadau mbalimbali kuhudumia meli tiba inayofahamika kwa jina la Jubilee Medical Boat, ambayo inasafiri kati ya visiwa vya Ziwa Victoria ikitoa huduma mbalimbali za afya.

"Pia GGML kwa kupitia fedha za Mfuko wa Uwajibika wa kampuni kwa jamii (CSR), mwaka jana ilisaidia ujenzi wa zahanati saba katika Halmashauri ya Mji wa Geita, kukamilika kwa idara 14 za wagonjwa wa nje na vituo vya afya vitatu, utoaji wa vifaa tiba pamoja na magari matatu ya kubebea wagonjwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

"Zaidi ya hayo kampuni yetu pia imesaidia kukamilika kwa idara tano za wagonjwa wa nje katika Wilaya ya Mbogwe na moja ya ziada Bukombe," alisema.

Aliongeza kuwa takribani muongo mmoja, kampuni ya GGML kwa kushirikiana na kampuni ya Rafiki Surgical Mission kutoka Australia ilisaidia kutoa upasuaji bure kwa takriban watu wazima na watoto 2,000 kutoka vijiji mbalimbali mkoani Geita ambao walizaliwa na tatizo la mdomo sungura.

"Oktoba mwaka jana, GGML ilitia saini mkataba wa makubaliano wenye thamani ya Dola za Marekani 120,000 ili kuongeza msaada kwa boti au meli ya matibabu kwenye Ziwa Victoria ambapo ufadhili wa GGML utadumu tena kwa miaka mitano ijayo hadi 2026," alisema.

Aidha, aliishukuru CCBRT kwa kuwa mshirika wa kweli wakati kampuni hiyo ikiendelea kutoa huduma maeneo mbalimbali nchini.


"Kampuni ya AngloGold Ashanti kupitia GGML tunashirikiana kila mara na mashirika yenye malengo kama yetu ili kuboresha na kuhakikisha huduma bora za kijamii zinawafikia watanzania wote.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Huduma za kitabibu katika Hospitali hiyo ya CCBRT, Dk. Cyprian Ntomoka, alisema msaada huo utaendelea kuboresha utoaji wa huduma za hospitali hiyo ambazo hugusa maisha ya watu duni wenye ulamavu wa aina mbalimbali.

"Tunatoa huduma kwa kinamama wajawazito wenye matatizo mbalimbali kama vile ulemavu. Tunatoa huduma kwa wanawake wenye matatizo ya fistula.

"Kwa hiyo GGML imetuongezea wigo mpana wa kutekeleza malengo ya CCBRT kutoa huduma kwa watu wengi zaidi.

"Pia kuna wale wenye matatizo sugu ya fistula ambayo yamewasababishia kupoteza watoto wawili au watatu. Hao pia tunawahudumia. CCBRT tupo kwa ajili ya kuwapatia huduma wale watu maskini ambao hawana uwezo wa kupata huduma za kiafya," alisema.




Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Kampuni ya GGML, Stephen Mhando (kulia), akikabidhi hundi ya Sh. milioni 50 iliyotolewa na kampuni hiyo kuunga mkono juhudi za Hospitali ya CCBRT katika utoaji huduma za afya ya uzazi. Kushoto na Mkurugenzi wa Huduma za Kitabibu katika hospitali hiyo, Dk. Cyprian Ntomoka na katikati ni Mkuu wa Idara ya Masoko na Wateja kutoka CCBRT, Sophia Shuma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazazi watakiwa kuwakumbusha wanafunzi elimu

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WAZAZI na walezi wilayani Bukoba mkoani Kagera kwa ushirikiano na walimu wametakiwa kuwakumbusha wanafunzi wa kidato cha sita kutambua kuwa nafasi waliofikia ndiyo msingi wa kujiunga na elimu ya juu ili kuaminiwa katika ajira.

Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Mosses Machali, mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na wazazi wa wanafunzi katika shule binafsi ya Kaizirege na Kemebozi baada ya kupewa taarifa ya elimu na matarajio yanayopangwa kufanyika.

Alisema bado safari ya elimu inaendelea katika vyuo vikuu ambavyo vinatoa falsafa mbalimbali na kumjenga mhitimu katika ubobezi.

Alisema, hatua inayotakiwa kufanyika sasa ni kujikumbusha katika masomo yanayotolewa darasani ili mitihani ya kipimo cha kufikia elimu ya juu ikitolewa iweze kuleta matokeo mazuri.

"Kwa sasa msilizike na nyie wazazi msione kwamba mtoto akimaliza kidato cha sita ndiyo msomi tayari, haitoshi kuwa mwanataaluma bali amepewa ujuzi wa kumvusha alipo na sasa ni mwendeleo wa kutafuta taaluma zaidi," alisema Machali.

Aidha, alisema muda wanaoutumia shuleni uwe kama aliyetumwa na kijiji kwenda kusoma na akili ifikirie kufika chuo kikuu.

Awali akisoma taarifa ya elimu na matarajio yatakayofanywa na shule hizo, Meneja wa Shule ya Uerogius Katiti alisema, kupitia Bodi ya Shule chini ya mkurugenzi wake, Yuston Kaizirege, imeinua kiwango cha elimu mkoani Kagera.

# Kampeni hedhi salama yawafikia yatima

**Halfan Chusi**

TAASISI ya Forward Motion inayojihusisha na utoaji na uhamasishaji wa elimu ya afya ya uzazi na hedhi salama kwa kushirikiana na madaktari bingwa, wametoa elimu kwa mabinti wanaolelewa kwenye vituo vya yatima jijini Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Forward Motion, Vivian Sirikwa, alisema wameamua kutoa elimu hiyo kwa mabinti hao ili kuwakinga na changamoto mbalimbali za afya ya uzazi na hedhi salama inayoweza kuwakuta kwenye mazingira wanayoishi.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa amesema kabla ya mafunzo hayo walifanya utafiti na kubaini kuwa wanawake wengi nchini hawatumii taulo za kike za kisasa wakati wa hedhi ndipo wakaanzisha kampeni iitwayo Tupa Kitambaa Jali Afya Yako kwa ajili ya kuhamasisha matumizi hayo.

"Hii ni kampeni inayohamasisha matumizi ya taulo za kike za kisasa kwa maana utafiti wetu umebaini kuwa asilimia 27 ya wanawake wa Kitanzania ndiyo wanaotumia taulo za kike za kisasa na wengine wote wakati wa hedhi wanatumia vitambaa ambavyo si salama kiafya," alisema.

Aidha amesema katika kutambua hilo wameamua kuungana na mabinti hao yatima ili kuwapa elimu ya afya ya uzazi na hedhi salama ili wakawe mabalozi wa kutoa elimu hiyo kwa mabinti wenzao na wanawake wengine kwa ujumla.

Pamoja na elimu hiyo taasisi hiyo imetoa msaada wa vyakula kwa watoto hao kwa ajili ya kutumia katika mfungo mtukufu wa Mwezi Ramadhani.

Akizungumza kwa niaba ya walezi wa vituo hivyo, Ustaadh Abdallah Abuu, kutoka Kituo cha Al Hidaya cha Buguruni, jijini Dar es salaam, ameishukuru Taasisi ya Forward Motion kwa kuwapa mabinti hao elimu ambayo imewafanya wajitambue zaidi na kuweza kuwa mabalozi kwa wengine.



Kiongozi wa ODM, Raila Odinga (kulia), aliyeambatana na Gavana wa Kaunti ya Pokot Magharibi, John Lonyangapuo, wakati wa mkutano wa Muungano wa Azimio la Umoja-One Kenya, Ortum, juzi. **PICHA: NATION MEDIA GROUP**

UCHAGUZI MKUU KENYA 2022:

# Raila avamiwa kwenye kampeni

**Uasin Gishu,** KENYA

RAILA Odinga anayewania urais kupitia Azimio La Umoja One Kenya amelaumu shambulio dhidi yake akiwa katika helikopta eneo la Kabenes, Kaunti ya Uasin Gishu.

Raila ameendelea kampeni kuelekea uchaguzi mkuu Agosti mwaka huu.

Amesema kundi la vijana lilimvamia wakati akiondoka eneo hilo kuelekea Ortum, Alale na Lomut, kuendelea na kampeni.

Amedai kwamba mawe yalirushwa akiwa pamoja na ujumbe wake.

Amesema hata wakati akielekea kupanda helikopta mawe yaliendelea kurushwa.

"Sisi hatujapiga mtu yeyote. Wala hatujafanya fujo pahali popote, tunalaani. Jana mimi nimeona vioja. Vijana wanakuja sisi tulitoka kutoa pole kwa familia halafu wakaanza kupiga magari yetu mawe.

"Mawe yalinyesha kama mvua kwenye gari langu. Wakipiga, nikauliza ni nini kinafanyika. Vijana walingojea nikiingia kwenye ndege halafu nikaona mtu anarusha mwamba mkubwa na sikuwa na pahali pa kwenda. Nilishangaa, ni mambo gani haya. Jamaa walitaka kutuua sisi."

**Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao**

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE

# Vituo vya mafuta, Bandari ya Odesa vyalengwa

• Putin kuuza gesi, mafuta kwa thamani ya pesa yake 'rubles'

**Odesa,** UKRAINE

MJI wa bandari, Odesa mapema jana asubuhi umeshambuliwa na vikosi vya Russia, ikisema inalenga vituo vya mafuta katika eneo hilo, ambalo Ukraine ilikuwa ikitumia kuwasafirisha wanajeshi wake.

Russia, imeelekeza zaidi nguvu zake za kivita kuelekea Mashariki mwa Ukraine, baada ya msururu wa vikwazo hasa karibu na mji mkuu wa Kyiv.

Maofisa wa Ukraine wanasema hakuna majeruhi walioripotiwa.

Wizara ya Ulinzi ya Russia, inasema kwamba vikosi vyake viliharibu kinu cha kusafisha mafuta na hifadhi tatu za mafuta zenye usawa wa juu wa makombora ya baharini na angani katika eneo la Odesa, shirika la habari la Interfax linaripoti.

Kwamba vifaa hivyo vilikuwa vinatumiwa na Ukraine kuwasafirisha wanajeshi wake karibu na mji wa Mykolaiv.

Odesa imekuwa ikijiandaa kwa mashambulio kwa wiki kadhaa, huku meli za kivita za Russia zikizunguka pwani ya Bahari Nyeusi.

Moshi ulionekana ukitanda mji huo wa kimkakati katika pwani ya Bahari Nyeusi jana, mashuhuda waliliambia shirika la habari la Reuters.

Anton Herashchenko, Mshauri wa Waziri wa Mambo ya Ndani wa Ukraine, amethibitisha kwenye chaneli yake ya Telegram kwamba Odesa ilishambuliwa kutoka angani, kwa makombora ambayo baadhi anasema yalidunguliwa na ulinzi wa anga.

### WAPATANISHI WAPIGANIA MAZUNGUMZO

Mpatanishi Mkuu wa Ukraine amesema kwamba mazungumzo yameendelea na kwamba Rais Volodymyr Zelensky anaweza kuzungumza na mwenzake wa Russia, Vladimir Putin.

Davyd Arakhamia anasema kuwa hatua zimepigwa katika mazungumzo kati ya wajumbe kwa njia ya video siku ya Ijumaa, akisema Russia imekubali mapendekezo ya Ukraine kuhusu masuala yote isipokuwa Crimea, eneo ambalo Russia ilinyakua kutoka Ukraine mwaka 2014.

Nyaraka za rasimu katika hatua hiyo, zinasema kwamba marais hao wawili wangeweza kufanya mashauriano moja kwa moja, lakini kazi ilikuwa ikiendelea katika masuala kadhaa mbali na waraka wenyewe. Russia, haijatoa tamko lolote kuhusiana na suala hilo.

Mpatanishi Mkuu kutoka Russia, Vladimir Medinsky, anasema baada ya mazungumzo ya Ijumaa misimamo yao kuhusu Crimea na Donbas haijabadilika.

Russia inasisitiza kwamba Ukraine itambue Crimea kama Russia, na kutambua uhuru wa Donbas, ambapo waasi wanaoungwa mkono na Russia wanadhibiti sehemu kubwa ya eneo.

### DONBAS YALENGWA BAADA YA KYIV

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky ameonya kwamba Russia, inataka kuteka maeneo ya Mashariki na Kusini mwa Ukraine.

Katika hotuba ya video usiku wa Jumamosi, amesema: Je, lengo la wanajeshi wa Russia ni nini? Wanataka kunyakua Donbas Mashariki na Kusini mwa Ukraine.

"Lengo letu ni nini? Tujilinde, tulinde uhuru wetu, ardhi yetu na watu wetu."

Zelensky pia amepongeza vikosi vya Ukraine vinavyolinda bandari ya Kusini ya Mariupol iliyozingirwa.

Upinzani wa Ukraine huko Mariupol na miji mingine ya Ukrane uliruhusu Kyiv kupata wakati kujiimarisha, na kusaidia kudhoofisha uwezo wa kijeshi wa Russia, rais huyo amesema.

Mapema wiki hii, Russia ilitangaza kwamba itapunguza kwa kiasi kikubwa karibu na mji mkuu wa Kyiv na mji wa Kaskazini mwa Chernihiv, na badala yake kuzingatia maeneo ya Mashariki mwa Ukraine.

### RUSSIA KUUZA GESI KWA PESA YAKE

Rais Putin amesaini amri kwamba kuanzia Aprili Mosi, mwaka huu, makampuni kutoka nchi zisizo mrafiki zake, wanapaswa kufungua akaunti ya ruble katika benki ya Kirussia na kisha kulipa ununuzi wa gesi ya nchi hiyo kupitia akaunti hiyo.

Vinginevyo, itazingatiwa kama uvunjaji wa mkataba na upande wa Russia, na wasambazaji wa Kirussia, wataacha kusambaza gesi asilia.

Takriban asilimia 40 ya gesi asilia ya Umoja wa Ulaya (EU) na asilimia 30 ya mafuta yake yanatoka Russia.

Ikiwa Russia itakatiza usambazaji, itakuwa ngumu kwa nchi za EU kupata njia mbadala kwenye soko la kimataifa.

Russia kwa sasa inapata euro milioni 400 kwa siku kutokana na mauzo ya gesi kwenda EU.

"Hatutoi bidhaa yoyote kwa mtu yeyote bure, na hatufanyi hisani," Putin amesema.

Makampuni na serikali za Magharibi zimekataa madai ya Russia, kulipa gesi kwa rubles, wakisema kuwa inakiuka mikataba iliyopo, ambayo inauzwa kwa euro au dola.

Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz amesema makampuni ya Ujerumani yataendelea kulipia gesi ya Russia kwa euro kama ilivyoainishwa kwenye mkataba.

HABARI MICHEZO

# KOCHA MBEYA CITY AANIKA TATIZO LA WACHEZAJI BONGO

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, amewashtukia wachezaji wa Kitanzania akidai kuwa wakipata ushindi mfululizo wana tabia ya kubweteka na kushindwa kupambana.

**Kocha huyo alisema hayo ikiishuhudia timu yake juzi ikilambwa bao 1-0 nyumbani, Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, akidai kuwa ameliona tatizo hilo kwa wachezaji wengi wa Kitanzania na si kwenye timu yake tu.**

"Nimeliona tatizo kwa wachezaji wa Kitanzania, wakishinda mechi mfululizo, basi wanabweteka na kuondoa ule moyo wa kupambana, wakidhani wanaweza kuendelea kushinda tu, hilo ndilo linaloendelea kwenye timu yangu," alisema kocha huyo raia wa Uganda.

Alisema mechi hiyo ilikuwa nzuri, lakini walifanya kosa moja ambalo lilitumiwa vizuri na wapinzani wao dakika ya 14, na muda uliobaki wachezaji wake walipambana kushambulia na kupiga krosi za kufunga bila mafanikio.

"Geita Gold ina wachezaji wazuri ambao wengi ni wazoefu kwenye Ligi Kuu na wameshacheza katika klabu kubwa, lakini hawana viungo wazuri, kwa hiyo niliingia na mfumo wa kuchezesha viungo wakabaji wawili, Samson Madeleke na Aziz Andambwile, lakini baada ya kuumia Aziz, ilibidi nibadilishe mfumo, hiyo nayo ilichangia. Lakini ukweli unabaki pale pale kuwa wachezaji wetu huwa wanabweteka sana," alisema.

Ni mechi ya sita mfululizo kwa Mbeya City kucheza bila kushinda tangu ilipoifunga Ruvu Shooting bao 1-0 Januari 20, mwaka huu, ikifungwa tatu na sare tatu, huku ikipoteza mechi mbili mfululizo nyumbani.

Kabla ya hapo ilikuwa na mwendelezo mzuri wa ushindi na kufanya vema kwenye Ligi Kuu ikiwamo kuifunga Simba bao 1-0 Januari 17 na kuilazimisha suluhu Yanga, Februari 5, mwaka huu.

Kabla ya mechi ya juzi, Machi 12 ilichapwa nyumbani bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar.

YA RAIS HII...



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, akipokea tuzo kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kutoka kwa Katibu wa Chama cha Muziki wa Dansi Tanzania (CHAMUDATA), Hassan Msumari, ambaye aliliwakilisha Shirikisho la Muziki Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Jamhuri yapanda Ligi Kuu Zanzibar*

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

TIMU ya Jamhuri, imesema itaanza maandalizi yake mapema kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Zanzibar ili kuweza kufanya vizuri.

Jamhuri imepanda daraja msimu huu, hivyo ujao wa 2022/23 itacheza Ligi Kuu Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Jamhuri SC, Abdullah Mohd 'Elisha', alisema wataanza mipango yao mapema ikiwamo kukiandaa kikosi chao kuelekea msimu wa 2022/2023 ili wasifanye makosa yaliyosababisha hadi kushuka daraja msimu uliopita.

Alisema miongoni mwa mipango yao ni kuongeza nguvu kwa kuwasajili wachezaji watano mpaka saba wenye uzoefu mkubwa kipindi tu dirisha la usajili litakapofunguliwa.

Elisha alisema licha ya kutarajia kuongeza nguvu kikosi chao, wataendelea kuwathamini na kuwajali wachezaji ambao wameipandisha daraja timu hiyo.

"Tutaongeza nguvu kikosi chetu ili kukamilisha mipango yetu ya kufanya vizuri katika ligi, lakini haimaanishi kuwa kuongeza kwetu nguvu ya wachezaji tutawasahau walioipandisha timu daraja, wachezaji hawa wanahitaji kutunzwa kwa walichokifanya," alisema.

Aidha, aliwaomba wadau wote wa timu hiyo kurudi na kuisaidia timu yao ili ifanikishe lengo lake ikiwamo kusaidia michango midogo midogo ya uwendeshaji timu hiyo

Hata hivyo, aliwapongeza wachezaji wote wa timu hiyo pamoja na benchi lao la ufundi kwa kazi nzuri waliyofanya mpaka kufanikiwa kupanda daraja.

## TSC Queens sasa kuja kivingine

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa TSC Queens, Hassan Hossam, amesema licha ya timu yake kutopata matokeo mazuri mzunguko wa kwanza, ameahidi duru la pili watafanya maajabu katika michezo iliyopo mbele yao.

TSC Queens imepoteza michezo yote 11 na kufungwa jumla ya mabao 43 kwenye mzunguko wa kwanza, hivyo kuifanya kuburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu ya Wanawake inayojumuisha timu 12 msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hossam alisema baada ya kupoteza michezo 11 ya mzunguko wa kwanza, walikaa na kufanyia kazi mapungufu yao na duru la pili wanakuja kivingine kuhakikisha wanapata matokeo katika michezo ijayo.

Alisema wanakwenda kupambana ili kubaki kwenye ligi na ili wasishuke ni lazima wapate pointi 15, jambo linawezekana kwa sababu ya mpango kazi atakaokuja nao.

"Tunaenda kufanya maajabu kwenye mzunguko wa pili, hatutakubali kufungwa kizembe kama ilivyo kwa duru la kwanza, tunahitaji pointi 15 katika michezo 11 iliyobaki ili kuhakikisha tunaendelea kubaki Ligi Kuu msimu ujao" alisema kcha huyo.

Alisema mzunguko wa pili wanakuja kivingine kuhakikisha hawapotezi mechi katika michezo 11 na kupambana timu hiyo iendelea kuwapo katika mikiki ya ligi hiyo.

## JKT Tanzania yaota Ligi Kuu

Na Adam Fungamwango

KOCHA Mkuu wa JKT Tanzania, Abdallah Mohamed 'Bares', amesema watapambana kufa kupona kwenye Ligi ya Championship ili kuhakikisha wanapata nafasi ya kurejea kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Bares ametoa kauli hiyo wiki iliyopita na kufafanua kuwa wanachofanya ni kuhakikisha wanashinda kila mchezo, halafu baadaye ndiyo wapige mahesabu ya kujua wako wapi na wafanye nini, lakini lengo ni kuhakikisha wanarejea tena Ligi Kuu.

Alisema hayo baada ya kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya African Sports kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

"Tuliwaandaa vijana vizuri sana, mechi hii ilikuwa muhimu kwetu kupata matokeo kutokana na jinsi msimamo ulivyo. Kwa sasa muhimu ni kushinda iwe nyumbani au ugenini, halafu mwisho ndiyo tutaangalia tuko kwenye nafasi gani, lakini lengo kubwa ni kutaka kurudi Ligi Kuu," alisema Bares.

## ZISIKUPITE

### SALAH KUJIFUNGA LIVERPOOL

MSHAMBULIAJI wa Misri, Mohamed Salah, 29, anakaribia kukubali mkataba mpya utakaomweka Liverpool hadi mwisho wa maisha yake ya soka. ***(Sunday Mirror)***

### LEWANDOWSKI AITAKA BARCA

STRAIKA wa Bayern Munich, Robert Lewandowski, 33, ameiambia Barcelona anataka kujiunga nayo kipindi cha majira ya joto, kama wataweza kutoa ofa nzuri kwa nyota huyo wa Poland ambaye mkataba wake umebaki miaka miwili. ***(Sport)***

### KANTE AWANIWA MADRID

REAL Madrid ni miongoni mwa klabu zinazomwania kiungo wa Chelsea, N'Golo Kante, 31, kama Mfaransa huyo atapatikana kipindi cha majira ya joto. ***(AS)***

### CHRISTENSEN FRESH BARCA

MLINZI wa Chelsea na Denmark, Andreas Christensen, 25, amefikia makubaliano ya awali ya kujiunga na Barcelona. ***(Football Insider)***

### ORIGI ANUKIA AC MILAN

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Divock Origi, 26, anakaribia kukubali mkataba wa miaka minne kujiunga na AC Milan. ***(Calciomercato)***

### HAG KUONDOKA NA WA2 AJAX

ERIK ten Hag tayari ametoa orodha ya wachezaji wawili wa kwanza atakaowasajili kama akiwa kocha wa Manchester United, wote kutoka kwenye klabu yake ya sasa ya Ajax, Winga wa Brazil, Antony, 22, na mlinzi wa kati wa Uholanzi, Jurrien Timber, 20. ***(Sunday Mirror)***

### GAVI MKATABA MREFU

KLABU za Manchester City na Liverpool zimeambiwa kwamba, kiungo wa Hispania, Gavi, 17, anatarajia kusaini mkataba mpya wa muda mrefu pale Barcelona. ***(90min)***

### RICE AWANIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL inataka kumsajili kiungo wa kati kipindi cha majira ya joto na anayewaniwa zaidi ni Declan Rice, 23, wa West Ham. ***(Football Insider)***

### MADDISON KUPELEKWA SOKONI

LEICESTER City inafikiria imuuze kiungo wake, James Maddison, 25, kwa pauni milioni 50, ili kukiboresha kikosi chao kipindi cha majira ya joto. ***(Mail on Sunday)***

### JOHNSTONE AGOMBEWA EPL

NEWCASTLE, West Ham na Southampton zote zinawania kumsajili nyota wa West Brom, Sam Johnstone, 29, na sasa Tottenham wameingia kwenye mbio hizo za kumtaka kipa huyo. ***(Mail on Sunday)***

### ARAUJO KUFUNGWA ZAIDI

BARCELONA pia ina matumaini ya kufikia makubaliano ya kuongeza mkataba na Ronald Araujo, 23, wiki ijayo wakiwa wanajua kwamba, mlinzi huyo wa kati wa Uruguay amepata ofa kutoka klabu za Ligi Kuu England. ***(Sport)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP: HATUTOI HATA INCHI MOJA MBIO ZA UBINGWA EPL

●●● Lazima tushinde michezo yetu, vinginevyo itakuwa ngumu na mechi ijayo ni dhidi ya City, hivyo...

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp anajua ni lazima timu yake iendelee kushinda ili kuweka hai mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England baada ya kupata ushindi wa 10 mfululizo wa ligi wakicheza dhidi ya Watford, Jumamosi.

'Wekundu' hao waliibuka kileleni mwa msimamo wa ligi kwa muda mfupi baada ya ushindi wa mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Anfield shukrani kwa bao la kichwa la Diogo Jota kipindi cha kwanza na mkwaju wa penalti wa dakika za lala salama kutoka kwa Fabinho.

Klopp alikiri kwamba swali lolote kuhusu kusonga mbele ya Manchester City kwa pointi mbili litakuwa batili baada ya kugundua vijana wa Pep Guardiola walikuwa tayari wameshatangulia kwa Burnley kabla hata hajaanza mkutano wake na wanahabari baada ya mchezo huo.

**Mabingwa hao watetezi, ambao watakuwa wenyeji wa Liverpool, walifanikiwa kushinda 2-0 wakiwa kwenye Uwanja wa Turf Moor.**

Klopp aliwaambia waandishi wa habari: "Hapana, huwezi kutoa hata inchi moja, lakini haihusiani na kuwa juu ya meza, sikufikiria juu ya hilo kwa sasa, nilikuwa na furaha kushinda mchezo na kuwa na pointi 72.

"Ili kuendelea na mbio za ubingwa, lazima tushinde michezo yetu, vinginevyo itakuwa ngumu sana. Na mchezo ujao wa Ligi Kuu ni dhahiri utakuwa mkubwa (dhidi ya City), hatujifichi kwa hilo. Yote ni nzuri.

"Sasa tuna mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambayo ni muhimu vile vile, na muda wa siku tatu kutayarisha hilo. Kisha tunatoka hapo."

Liverpool hawakuwa katika kiwango bora dhidi ya 'Hornets' hao, lakini walijihakikishia pointi tatu.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
CRYSTAL PALACE
VERSUS
ARSENAL
1 | 3.67
X | 3.23
2 | 2.05

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# RANGNICK ASIFU KIWANGO CHA MAGUIRE MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

RALF Rangnick alitaja uchezaji wa Harry Maguire katika sare ya bao 1-1 kati ya Manchester United na Leicester City "usio na dosari" baada ya beki huyo kuzomewa alipokuwa akiichezea England, huku Bruno Fernandes akisema vyombo vya habari vilihusika kwa kiasi fulani.

Kocha huyo wa muda wa United, Rangnick pia alisifu mapokezi aliyopewa Maguire na mashabiki wa Old Trafford, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, akizomewa wakati wa mechi ya kirafiki ya England dhidi ya Ivory Coast, Jumanne.

Maguire amekosolewa kutokana na uchezaji wake katika safu ya ulinzi ya United ambayo imecheza mechi saba pekee bila kuruhusu nyavu zake kutikiswa kwenye Ligi Kuu England msimu huu, idadi ambayo ni mbaya zaidi kuliko timu tisa za ligi hiyo.


Rangnick, hata hivyo, alifurahishwa na kiwango cha Maguire dhidi ya timu yake hiyo ya zamani, Jumamosi.

"Mwitikio wa mashabiki wetu (kwa Maguire) ulikuwa kama kawaida," alisema Rangnick akiiambia Sky Sports.

"Ni mojawapo ya (mashabiki) bora zaidi, kama si bora zaidi, nchini England.

"Harry alicheza vizuri, alikuwa na mchezo usio na dosari leo kwa kujilinda. Ulikuwa mchezo mzuri kutoka kwake."

Kiungo Fernandes alimtetea mwenzake, akidai vyombo vya habari ndivyo vimekuwa vikikuza mambo kuhusu kiwango cha Maguire na ndivyo vilichangia kejeli zilizosikika kwenye Uwanja wa Wembley.



# 'Joao anafanya kila kitu Atleti'

**MADRID,** Hispania

JOAO Felix 'aliyefufuka' anafanya kila kitu ambacho Atletico Madrid wanakitaka, kwa mujibu wa Kocha Mkuu, Diego Simeone.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno, aliendelea na kiwango chake bora Jumamosi kwa kufunga mabao mawili huku mabingwa hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, wakiambulia ushindi mnono wa mabao 4-1 dhidi ya Deportivo Alaves.

Joao sasa amehusika katika mabao nane katika michezo yake sita iliyopita katika mashindano yote (mabao sita, asisti mbili), ambayo ni sawa na michezo yake 33 kabla ya hapo (mabao manne, asisti nne).

Simeone amefurahishwa na mchango wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, na anaamini kuwa yuko kwenye njia sahihi baada ya kile ambacho kimekuwa mbali na kazi nzuri ya Atleti hadi sasa, tangu aliposajiliwa kwa fedha nyingi kutoka Benfica mwaka 2019.

"Anaendelea kukua, yuko katika wakati mzuri," alisema Simeone akiiambia Movistar+.

"Ana furaha. Yuko sawa na anafanya kila kitu tunachohitaji kutoka kwake."

## HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# NYOTA WA TEMBO WARRIORS AULA YEDITEPE YA UTURUKI

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Tanzania ya Watu wenye Ulemavu, 'Tembo Warriors', Alfan Kiyanga, amesaini mkataba wa miaka miwili kucheza soka la kulipwa na Klabu ya Yeditepe inayoshiriki Ligi Kuu ya Watu wenye Ulemavu nchini Uturuki.

Kiyanga ambaye ametokea katika Klabu ya LSL Amputee FC inayoshiriki Ligi Kuu ya Walemavu Tanzania, baada ya kusaini mkataba huo, juzi aliichezea timu hiyo mechi yake ya kwanza na kuisaidia kuibuka na ushindi wa bao 1-0, lililopatikana kwa mkwaju wa penalti, ambayo aliisababisha yeye.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Shirikisho la Soka kwa Watu wenye Ulemavu nchini (TAFF), Mosses Mabula, alisema wamepokea taarifa kutoka Klabu ya Yeditepe kwamba wameridhishwa na uwezo wa nyota huyo na kumsainisha mkataba wa miaka miwili.**

Alisema ni jambo la kujivunia kwa taifa kuendelea kupata ongezeko la wachezaji wa timu ya Tembo Warriors kwenda kucheza soka la kulipwa nchini Uturuki.

"Ni jambo zuri na tunajivunia kama nchini, ukizingatia hivi karibuni tunatarajia kwenda kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia na itachezwa Uturuki, kupata nafasi ya kucheza huko kunasaidia nyota wetu kupata uzoefu mkubwa ikiwamo kuzoea hali ya hewa na mazingira," alisema Mabula.

Alisema kupata nafasi kwa mchezaji huyo pamoja na wengine watatu ni mwanga mzuri kwa Tembo Warriors kuweza kuzoea haraka uchezaji wa wachezaji wa Uturuki hasa watakapokwenda katika fainali za Kombe la Dunia Oktoba mwaka huu.



Mchezaji wa Timu ya Mpira wa Kikapu ya JMK, Paul William, akijaribu kutumbukiza mpira kwenye nyavu huku akizongwa na wachezaji wenzake wakati wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Taifa Stars imeniongezea vitu - Mpole

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA tegemeo wa Geita Gold, George Mpole, amesema kuitwa kwake timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars', kumemwongezea ufundi kwa kuwa mafunzo aliyoyapata ikiwa ni pamoja na kucheza mechi mbili za kimataifa dhidi ya Afrika ya Kati na Sudan, kumemfanya kuzidi kujiamini.

Mpole ambaye juzi aliifungia timu yake bao pekee, Geita Gold ikiiadhibu Mbeya City nyumbani kwao, Uwanja wa Sokoine bao 1-0, amesema anaamini atafanya vizuri zaidi ya mwanzo kwa sababu akiwa kwenye kikosi cha timu ya taifa, amejifunza vitu vingi ambavyo hakuwa navyo, hivyo kumwongezea uwezo.

"Nashukuru kwa kuifungia timu yangu bao pekee, unajua kwa sasa mimi ni mchezaji wa Taifa Stars kwa hiyo wachezaji wenzangu hapa wananiangalia mimi, hivyo ni lazima nipambane kwa kushirikiana nao ili kuwafanya na wao wajitume zaidi.

"Pia kuwapo kwenye kikosi cha timu ya taifa kumeniongezea vitu zaidi na naamini huu ni mwanzo tu, inabidi nipambane zaidi ili kufikia malengo na kwa mimi huu ndiyo mwaka wangu bora zaidi kwenye soka, nataka niendee kuwa hivi au zaidi," alisema.

Bao hilo linamfanya afikishe mabao tisa, nyuma ya vinara Fiston Mayele wa Yanga na Relaints Lusajo wa Namungo ambao wana mabao 10 kila mmoja.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 04/04/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 2105 | Tobol Kostanay vs FK Arys | 1.53 | 3.79 | 5.44 |
| 16:00 | 3145 | Tanzania Prisons vs Dodoma FC | 1.39 | 3.87 | 8.33 |
| 16:00 | 5723 | Bul FC vs Uganda Revenue Authority FC | 3.45 | 3.10 | 2.19 |
| 17:15 | 1419 | FK Vozdovac vs Radnik Surduluca | 1.70 | 3.45 | 4.48 |
| 17:30 | 3357 | Cherno More vs Botev Vratsa | 1.28 | 4.68 | 9.74 |
| 18:00 | 1526 | Vittoriosa Stars vs Rabat Ajax | 2.32 | 3.37 | 2.68 |
| 18:30 | 1558 | Skeid Fotball vs Stabaek | 3.31 | 3.46 | 1.97 |
| 19:00 | 1225 | Aasane Fotball vs IK Start | 2.48 | 3.31 | 2.53 |
| 19:00 | 1570 | Pafos FC vs AEK Larnaca | 2.64 | 3.19 | 2.64 |
| 19:00 | 1689 | Hapoel Kfar Saba vs Hapoel Petah Tikva | 2.27 | 2.94 | 3.44 |
| 19:00 | 1979 | Sogndal vs Raufoss | 1.70 | 3.74 | 4.08 |
| 19:00 | 3428 | Mjondalen vs Kongsvinger IL | 1.94 | 3.44 | 3.40 |
| 19:00 | 3770 | Hapoel Raanana vs Hapoel Ramat Gan | 2.64 | 2.84 | 2.94 |
| 19:00 | 3798 | Lokomotiva Zagreb vs Slaven Belupo | 2.11 | 3.21 | 3.17 |
| 19:00 | 4604 | Fredrikstad vs Stjordals-Blink | 1.44 | 4.38 | 5.64 |
| 19:00 | 5295 | Wisla Plock vs Gornik Zabrze | 2.44 | 3.22 | 2.63 |
| 19:30 | 3234 | Verona vs Genoa | 1.85 | 3.50 | 4.10 |
| 19:30 | 5626 | Proleter vs Cukaricki St | 3.79 | 3.21 | 1.91 |
| 19:45 | 5683 | Laval vs Sedan | 1.66 | 3.40 | 5.33 |
| 20:00 | 1927 | Midtjylland vs Silkeborg | 1.79 | 3.59 | 4.19 |
| 20:00 | 2247 | Landskrona Bois vs Osters IF | 2.58 | 3.08 | 2.88 |
| 20:00 | 2393 | IK Brage vs Orebro SK | 2.42 | 3.33 | 2.88 |
| 20:00 | 2640 | Lokomotive Sofia vs Tsarsko Selo | 1.73 | 3.40 | 4.38 |
| 20:00 | 3507 | Viktoria Berlin vs Magdeburg | 5.35 | 4.06 | 1.55 |
| 20:00 | 4996 | Elfsborg vs Mjallby | 1.51 | 4.00 | 5.27 |
| 20:00 | 5800 | Gais vs IK Oddevold | 1.43 | 4.47 | 5.64 |
| 20:10 | 4170 | Djurgardens IF vs Degerfors | 1.34 | 4.87 | 6.63 |
| 20:30 | 2934 | Maccabi Bney Reine vs SC Kfar Qasem | 2.18 | 3.11 | 3.46 |
| 20:30 | 3439 | Basaksehir vs Yeni Malatyaspor | 1.35 | 4.77 | 7.95 |
| 20:30 | 3831 | Maccabi Haifa vs Hapoel Beer Sheva | 2.11 | 3.30 | 3.11 |
| 20:30 | 4806 | Hatayspor vs Adana Demirspor | 2.73 | 3.33 | 2.45 |
| 21:00 | 1310 | Jong Ajax vs FC Oss | 1.51 | 4.54 | 4.94 |
| 21:00 | 2180 | CFR Cluj vs Argesul Pitesti | 1.48 | 3.71 | 7.53 |
| 21:00 | 2896 | Jong Utrecht vs NAC Breda | 3.01 | 3.55 | 2.12 |
| 21:00 | 3717 | Jong AZ Alkmaar vs Roda Kerkrade | 3.50 | 3.65 | 1.90 |
| 21:00 | 4211 | Jong PSV vs FC Volendam | 2.76 | 3.54 | 2.27 |
| 21:30 | 1452 | Sportivo Italiano vs Argentino Merlo | 2.11 | 3.15 | 3.60 |
| 21:30 | 1594 | Excursionistas vs Claypole | 2.35 | 2.85 | 3.40 |
| 21:30 | 1644 | Deportivo Espanol vs Deportivo Laferrere | 2.40 | 2.77 | 3.11 |
| 21:40 | 3199 | Deportivo Riestra vs CA Guemes | 2.43 | 2.72 | 3.11 |
| 21:45 | 1147 | Nancy vs AC Ajaccio | 3.56 | 2.87 | 2.22 |
| 21:45 | 1554 | UCD Dublin vs Derry City | 6.41 | 4.18 | 1.42 |
| 21:45 | 2275 | AC Milan vs Bologna | 1.36 | 4.81 | 7.81 |
| 21:45 | 5568 | Treaty United vs Athlone Town | 1.58 | 3.99 | 4.67 |
| 22:00 | 2718 | Real Sociedad vs Espanyol | 1.61 | 3.94 | 5.45 |
| 22:00 | 2922 | Crystal Palace vs Arsenal | 3.67 | 3.23 | 2.05 |
| 22:00 | 3794 | Leganes vs Fuenlabrada | 1.78 | 3.28 | 4.68 |
| 22:00 | 5055 | Finn Harps vs Drogheda Utd | 1.92 | 3.17 | 3.80 |
| 22:15 | 4191 | Porto vs Santa Clara | 1.24 | 5.57 | 10.94 |
| 22:45 | 2960 | CSD Barnechea vs Union San Felipe | 2.95 | 3.05 | 2.45 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Aprili 4, 2022

Nipashe




Rangnick asifu kiwango cha Maguire UKURASA 22

UMETISHA...



Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pauline Gekul, akimkabidhi Tuzo ya Mwanamuziki Bora wa Mwaka, Rajab Abdul Kahali 'Harmonize', baada ya kutangazwa mshindi katika hafla ya utoaji tuzo hizo iliyofanyika juzi jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Washindi Tuzo za Muziki 2021 waula

## ●●● Serikali yageukia maisha yao, sasa kukatiwa Bima za Afya na Pensheni huku...

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na michezo, Mohamed Mchengerwa, amesema serikali itawakatia Bima ya Afya washindi wote wa tuzo za muziki wa mwaka huu kwa muda wa mwaka mzima ili kuwaondolea adha ya kupata matibabu wakiwa katika shughuli zao za muziki ndani na nje ya nchi.

**Mchengerwa alitoa kauli hiyo wakati wa usiku wa kilele cha utoji wa Tuzo za Muziki 2021 kwenye Ukumbi wa kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam usiku wa kuamkia jana.**

Aidha, alisema serikali pia itawakatia pensheni wasanii wote washindi walioshinda tuzo hizo na kuwalipia kwa mwaka mzima ikiwa ni mwanzo wa kuwaanzishia mfumo wa kujiwekea akiba uzeeni ili kuwaondolea adha ya kuwa ombaomba pindi kipindi chao cha kazi kinapofikia ukingoni.

"Na hapa niseme tu ni lengo la serikali yetu ya awamu ya sita chini ya Uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha wasanii, wanamichezo na wadau wa sanaa wanawekewa mazingira mazuri ya ufanyaji kazi na mazingira mazuri ya hapo baadaye baada ya kustaafu kazi.

"Hivyo, licha ya zawadi hii ya bima na pensheni kwa washindi wa leo hapa, lakini tayari katibu mkuu, ameanza mazungumzo na taasisi zetu za bima na pensheni ili mwishowe wasanii, wanamichezo na wadau wetu wote wa tasnia za sanaa na michezo waweze kunufaika na bima na pensheni kwa njia rahisi ili kuyalinda maisha yao ya sasa na ya baadaye," Mchengerwa alifafanua.

Amelitaka Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), kutenda haki na kujiepusha na vitendo vya ukiukwaji wa maadili, sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na kwamba lisitumike kukandamiza haki zao na kuwagawa, hivyo kusababisha makundi miongoni mwao.

"Wito wangu BASATA ni chombo cha kuwaunganisha wasanii na kutetea haki na maslahi ya wasanii na kuwa kimbilio lao. Sitakubali kuona vitendo viovu vikiendelea wakati wa uongozi wangu nakataa na ninakemea," alisisitiza.

Kwa upande wa Taasisi ya Hakimiliki (COSOTA), Mchengerwa ameiagiza kuwasaidia wasanii kusajili kazi zao ili waweze kunufaika nazo.

Wakati huo huo, Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, Samia Suluhu Hassan, amepewa Tuzo ya Heshima kwenye usiku huo wa kilele cha utoaji wa tuzo za muziki Aprili 2, 2022 jijini Dar es Salaam.

Tuzo hiyo ya heshima amepewa na wasanii kwa kuthamini mchango wake mkubwa anaoutoa kwao.

Watu wengine waliopata tuzo za heshima katika usiku huo ni pamoja na Diamond Platnumz, Ruge Mutahaba, Bibi Kidude na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi nchini, Jenerali Venance Mabeyo.

Katika usiku huo, tuzo 51 zilitolewa ambapo nne ni za heshima na arobaini na saba ni za kupigiwa kura.

# Yanga sasa yaiandalia Azam FC mbinu mpya

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha inanyosha vema njia zake za kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara msimu huu, Klabu ya Yanga imedhamiria kuondoka na pointi tatu dhidi ya Azam FC, baada ya Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Cedric Kaze kueleza kwamba mechi hiyo kwao ni zaidi ya fainali na kwamba wataingia na mbinu mpya kwenye mchezo huo.

Yanga watakuwa ugenini kwenye mchezo huo utakaopigwa keshokutwa, Jumatano katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo Jiji la Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaze alisema mchezo huo utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu timu zote zinajuana, hivyo watahakikisha wanaingia kivingine ili kupata pointi zote tatu.

Alisema mechi hiyo wanakwenda kucheza tofauti nyingine licha ya ligi kuwa moja na kwamba hata maandalizi yake yamekuwa tofauti, lengo likiwa ni kupata matokeo chanya.

"Azam FC si timu ya kuibeza kwa sababu hawakupata matokeo mazuri katika mchezo wa mwisho walipocheza katika uwanja wao wa nyumbani, tutaingia kwa nidhamu na mbinu mpya ili kufikia malengo yetu ya kutafuta pointi muhimu katika mchezo huo," alisema Kaze.

Alisema wanafanyia kazi udhaifu uliojitokeza katika kikosi chao michezo iliyopita ikiwamo utulivu wa safu ya ushambuliaji na mabeki wake kuhakikisha wanatumia vizuri nafasi wanazotengeneza pamoja na kuwazuia washambuliaji wa Azam FC.



Kocha Cedric Kaze

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >